Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 76 No. 188 | JUMADIL AWWAL 1438 AH | FEBRUARI 2017 | TABLIGH 1396 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini! bila shaka vileo na kamari na masanamu (ya kuabudu) na mishale (ya ramli) ni uchafu wa kazi ya Shetani. Basi jiepusheni nayo, ili mpate kufaulu.
Hakika Shetani anataka tu kuunda uadui na bughudha kati yenu kwa njia ya vileo na kamari na kuwazuilieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusali. Basi je, mtaacha? (*5:91-92*)

Khalifa Mtukufu awakumbusha Waahmadiyya

Simamisheni Sala kwa kuzingatia adabu zake

**Na Mwandishi Wetu,
Dar es Salaam**

Baada ya kusoma Tashahhud, Tauz, Tasmia na Surat Fatihah, Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alisema:
Katika hotuba iliyopita nilielezea umuhimu wa sala na pia nikazungumzia juu ya kutekeleza sala kwa kudumu. Nimepokea barua kutoka kwa watu wengi ambao walikuwa wanaelezea hali zao na wanajutia juu ya madhaifu yao. Kutoka katika Jamaat nyingi na katika Tanzeem nimepokea barua ambazo zinaonyesha hali ya kukubali kuwa kwa hakika kulikuwa na udhaifu katika jambo hili. Njia madhubuti na thabiti zimeanzishwa, na Mungu akipenda, watajitahidi vya kutosha kuondoa madhaifu haya.
Mwenyezi Mungu Mtukufu awawezeshe kutekeleza yote hayo. Allah aiwezeshe misikiti yetu ibebe lile lengo la kweli la kuwepo kwake na iwe mifano bora kadiri inavyowezekana katika jambo hili. Ingawa uongozi unatakiwa uzingatie kwamba ili kupata matokeo mazuri, basi ni lazima mtu aonyeshe juhudi.
Ingawa mwanzoni kila mmoja kati yetu hulianza jambo hili kwa shauku na mapenzi makubwa, ijapokuwa baada ya muda kupita mtu anaanza kuonyesha hali ya kutojali. Jambo hili linapatikana katika asili ya mwanadamu. Ikiwa mtu atakuwa mzembe, na ingawa jambo hili linahitaji umakini na kisha halichukuliwi tahadhari, basi ikiwa uongozi utazembea, basi jambo hili litakuwa katika hali ya hatari. Ikiwa mfumo wa uongozi ulioundwa ili kuwakumbusha watu utazembea na utaonyesha hali ya kutojali katika majukumu yake, hali ya kuwabadili watu itakuwa ngumu sana, kwa sababu hali ya kutojali miongoni mwa watu inajitokeza kutokana

Endelea uk. 3



Sehemu ya waumini wakiwa ndani ya Msikiti wa Baitul Futuh mjini London tayari kusikiliza hotuba ya Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih V a.t.b.a.

Vita Dhidi ya Dawa za Kulevya:

Islam ndio inayotoa suluhisho la kweli

**Na Abdillah Kombo,
Dar es Salaam**

Misongo ya mawazo, umasikini, kukosekana kwa elimu ya kutosha katika jamii ni miongoni mwa sababu kubwa zinazopelekea wengi kujiingiza katika matumizi yasiyo sahihi ya dawa za kulevya nchini. Kauli hiyo imetolewa na Mtaalam bingwa wa afya ya akili Dr. Fileuka Ngakongwa alipokuwa akiongea na mwandishi wetu kuhusu tatizo kubwa la dawa za kulevya hapa nchini. Mtaalam huyo alisema kuwa, dawa hizi kwa kawaida zimegawanyika katika makundi makubwa mawili, kundi la kwanza ni zile ambazo mtu akitumia humfanya awe mchangamfu aliyepita kiasi. Na kama mtu kwa asili ni mwenye aibu, mpole au si muongeaje, basi dawa hizi zitamfanya awe na tabia tofauti kabisa na ile ya asili yake ya siku zote. Alisema wengi wa watumiaji wa aina hii ni watu wenye kipato kikubwa, wanamuziki nk na hii alisema ni kutokana na kuwa dawa hizi huuzwa ghali sana. Kwa watumiaji wa aina hii ya dawa huwafanya waweze kuchangamka na kufanya shughuli zao, kwa wanavyoamini wako kuwa ni kwa ufanisi zaidi. Mfano halisi wa dawa hizo katika kundi hili ni "Cocaine"



Rogers William Sianga, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya

Kundi la pili ni dawa zile zinazomfanya mtu apende kupumzika au kuliwazika tu muda wote. Watumiaji wa kundi hili ni watu wanaojiona hawana raha, misongo ya mawazo kichwani, kukosa utulivu nk, hivyo anapoamua kutafuta utulivu huo ndio hapo anapoamua kuanza kutumia dawa za kulevya. Shida ni kuwa baada ya muda mfupi sana akili yake itakuwa haiwezi tena kufanya lolote bila kutumia dawa hivyo, kwani kiasi alichoanza kutumia ili kupata faraja mara ya kwanza, kitaongezeka kwa haraka mno na hatimae kuwa hataweza kufanya kitu

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

MWANA ALIYEAHIDIWA r.a.

Hatuna kumbukumbu (lakini kama unayo utusaidie, kwani kwa kila anayejua yupo anayejua zaidi) ya binadamu yeyote aliyesimama kadamnasi bila woga wala hofu na kuwaambia walimwengu kuwa Allah Ameniahidi kunipatia mtoto mtakatifu na mzuri atanasibishwa na utukufu na utajiri, atakuwa na akili nyingi mno, atajulikana pembe zote za dunia, atawakomboa wote waliopo katika minyororo, atawafanya watatu kuwa wane, atajaaliwa elimu ya nje na ya ndani, sifa zote hizi zimetimia katika dhati ya mwana aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra).

Si rahisi kuzizungumzia sifa zote hizo kwa pamoja, lakini kwa leo tutajikita katika uwanja wa elimu na kuiona shani ya Allah Alivyoidhihirisha kwa kumpatia elimu mwana huyu aliyeahidiwa.

Sawa na jicho la kibinadamu mwana aliyeahidiwa hakuwa anafanya vizuri shuleni. Malalamiko yalifika kwa Masihi Aliyeahidiwa (as) naye akawaambia wamuache. Kwa ujumla masomo yake ya shuleni hayakuwa na lolote la kuleta matumaini. Tizama sasa yaliyotokea kwa huyu aliyekuwa hafanyi vizuri shuleni. Tizama vitabu alivyoviandika. Tizama hotuba alizozitoa. Tafakari juu ya ushauri aliyokuwa anawapa watu. Ni muujiza mkubwa wa kielimu. Ni vigumu kuzungumzia elimu aliyokuwa nayo mwana aliyeahidiwa. Tutakachofanya ni kutazama kitabu kimoja tu chake. Nacho ni "Maisha ya Mtume Muhammad (saw)". Kitabu hiki ni muujiza mkubwa. Mtu anaweza kupata hisia ya kwamba mwandishi alikuwa Uarabuni wakati wa enzi za Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Ubingwa wake mkubwa unajitokeza anavyoanza kitabu hicho kwa kuangalia historia ya Uarabuni kabla ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) hajazaliwa. Taratibu anakuvuta hadi kwenye mabadiliko makubwa yaliyoletwa na huyu mteule wa Allah. Jinsi gani alivyowabadili hao watu waliokuwa wanakunywa pombe mara tano wakawa sasa wanasali sala tano kila siku. Mwenendo wa Masahaba ukabadilika kabisa na lililobaki kwao ni moja tu "Kusikia na kutii".

Waandishi maarufu hususan wa Ulaya wamekisifu sana kitabu hiki na kushangaa ni jinsi gani mwandishi alivyoweka mizani katika kuwakilisha mawazo yake. Kuna Mwandishi mmoja aliwahi kusema ya kwamba "Hakuna kitabu kilichofanikiwa kuleta picha iliyokamilika ya maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kama kitabu hicho".

Lakini usisahau huyu ndiyo Yule ambaye hakupata elimu kama wanavyodhani wengi. Nini basi siri ya mafanikio yake? Katika safari yake ya London kueleza Islam kwa Uropa maadui wa Jumuiyya walifanya hila ya kumfedhehesha Mwana Aliyeahidiwa (ra). Maadui hao wakifahamu kiwango cha elimu cha Mwana Aliyeahidiwa (ra) waandishi wa habari waliambiwa wamuulize kuwa yeye amesoma chuo gani? Kwa upole bila jaziba na akiwa anafahamu makusudi yao aliwaambia; "Je mnafahamu chuo alichosomea Mtukufu Mtume Muhammad (saw)? Basi mimi nimesoma katika chuo hicho hicho". Jibu hili lilikuwa sahihi kabisa. Unaposoma vitabu vyake vingi unafika mahala ambapo anasema sikujua maana ya jambo hili au neno hili Malaika ndio wamenifundisha. Utashindana vipi na Yule ambaye anafundishwa na Malaika wa Allah? Ahadi ya kuwa na akili nyingi kwa hiyo inatokana na chimbuko la Mwana Aliyeahidiwa (ra) kuwa na waalimu na Waalimu wake walikuwa ni Malaika wa Allah.

Vita Dhidi ya Dawa za Kulevya:

Kutoka uk. 1

chochote tena bila kutumia hizo dawa. Mfano halisi hapa ni "Heroin" ambayo hata kwa bei, yenyewe ni nafuu kulinganisha na Cocain.

Mwili wa binadamu una mifumo mingi tofauti tofauti ya kumsaidia binadamu katika maisha yake ya kila siku, mifumo hii ni pamoja mifumo yenye kumpa binadamu hasira na faraja pia. Mojawapo ya mifumo unaojulikana kitaalam kama "Reward System" mfumo huu kwa asili yake hasa humpa binadamu faraja kwa kile kiasi ambacho kwa asili yake kinatakiwa kutoa kwa binadamu. Kwa maana hiyo basi, sehemu kubwa ya dawa hizi za kulevya huenda kuathiri mfumo huo na hivyo mtumiaji kujikuta anapata faraja iliyopitiliza tofauti na uhalisia wa mfumo wenyewe. Akili nayo hupenda kuliwazika na dawa hizi zina uwezo mkubwa mno wa kuiliwaza na kubadilisha mfumo wa akili ili kipaumbele cha kwanza kwa mtumiaji wa dawa hizi iwe ni kupata dawa atumie kwa njia yeyote ile alisisitiza mtaalam huyo. Alisema mtumiaji akisha kufikia hapo, basi ndio mashaka huanza, kwani kwa kiasi kikubwa sana atakuwa hawezi kufanya lolote bila ya kutumia hizo dawa, lakini baya zaidi ataanza sasa kujiingiza katika maswala ya uvunjifu wa amani, ikiwa ni pamoja na kuanza kuiba, kupokonya, kukaba nk ili tu ahakikishe anapata pesa za kununua na kutumia dawa hizi.

Aidha aliendelea kusema kuwa, yako mengi yanayoweza kufanywa ili kupunguza kama si kuondoa kabisa tatizo hili hapa nchini. Kwa maoni yake, alisema kuwa kuna haja sasa, maswala ya matumizi ya dawa za kulevya, athari zake na shida zake kwa mtumiaji kuanza kufundishwa mashuleni kuanzia kwenye ngazi za chini kabisa. Akiamini kuwa kama vijana wetu watapatiwa elimu na kuelewa shida na madhara ya kutumia dawa hizi, bila shaka itapunguza kwa kiasi kikubwa kwa wao wenyewe kutojiingiza katika kutumia dawa hizi.

Jambo jengine alishauri kuwa, wataalam wa afya ni bora kuanzia sasa katika ngazi za chini kuanza kuwauliza watu wanaotembelea vituo vya afya, kama wanatumia aina yeyote ya mihadarati, ili kama ikigundulika basi hatua za awali na za haraka ziweze kuchukuliwa kuwasaidia watu hao. Hapa aliunganisha na maduka ya dawa kuacha kuuza dawa kienyeji, bila kuwa na cheti cha daktari. Kwani kuna aina nyingi za dawa halali kabisa lakini zikitumika bila kufuata ushauri wa kitaalam huenda zikamfanya mtu kutumbukia katika shida hii ya kutumia dawa za kulevya.

Na mwisho alisema kama zilivyofanywa kampeni nyingi kuhusu balaa la ugonjwa hatari wa Ukimwi, basi hata kwenye hili tunaweza kufanya hivyo hivyo, kukawa na magari yanayotembea mitaani na kutoa elimu juu ya janga hili. Pia kuwepo vituo vingi kwenye maeneo ya karibu na watu, ili kutoa ushauri, mafunzo, nk. Vituo hivi visaidie pia kutoa ufumbuzi wa matatizo ya kijamii na ya kifamilia. Tukiweza kufanya haya, tutakuwa tumewapatia watu wetu elimu kuhusu madhara ya dawa hizi, tumewapunguzia misongo ya mawazo ambayo kwa kiasi kikubwa hupelekea watu kujiingiza katika utumiaji wa dawa hizi na kwa kuwa tutakuwa na watu waelewa na wenye siha, basi wataweza pia kufanya kazi na kujipatia riziki zao za halali. Alimalizia daktari huyo bingwa wa afya ya akili kutoka hospitali ya Taifa ya Muhimbili iliyopo jiji Dar es Salaam.

Kwa mtazamo wa Kiislam, dawa za kulevya (ulevi) ni moja kati ya tatizo kubwa linaloikabili dunia ya leo. Kutokana na kuenea mno kwa vileo vijana wa Kiislam na wengine kwa ujumla wanabaki njia panda, baadhi wakiwa hawaelewi ni kwa kiwango gani Uislamu umekataza au kuharamisha matumizi ya ulevi na umeweka mkazo wa kiasi gani juu ya kutokutumia ulevi.

Ndani ya Quran tukufu Mwenyezi Mungu Anatuambia:

Enyi mlioamini! bila shaka vileo na kamari na masanamu (ya kuabudu) na mishale (ya ramli) ni uchafu wa kazi ya Shetani. Basi jiepusheni nayo, ili mpate kufaulu.

Hakika Shetani anataka tu kuunda uadui na bughudha kati yenu kwa njia ya vileo na kamari na kuwazuilieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusali. Basi je, mtaacha? (5:91-92)

Sawa na aya hizi ulevi umefananishwa na kamari na kuabudu masanamu na umetajwa kuwa ni kazi za shetani. Mwenyezi Mungu Anatutahadharisha kujiepusha na ulevi kwamba shetani anakusudia kujenga audui na bughudha baina yetu kwa kupitia ulevi na baya zaidi anakusudia kutusaulisha lengo kubwa la kuumbwa kwetu ambalo ni kumwabudu Allah kunakotakiwa kuonyeshwe kwa njia ya kusali na kumkumbuka Allah.

Kuna hasara na madhara mengi sana ya ulevi yakiwemo yale ya kimwili, ya kiakili, kiuchumi, kijamii, kiustaarabu, kiusalama, amani na maendeleo ya kiroho.

Ni muhimu sana ikumbukwe kwamba sawa na mafundisho ya Islam, neno ulevi au kileo linaingiza kila kitu kinacholevya ambacho kinapelekea msisimko usio wa kawaida wa mwili na hivyo kumfikisha mtu kwenye kupoteza fahamu yake au kukosa umakini, kukosa kujitambua na kujidhibiti 'self-control'. Vileo vinavyoweza kutajwa kwa haraka ni kama vile aina zote za pombe za viwandani, aina zote za pombe za kienyeji, bangi na mti wowote unaolevya, jamii yote ya cocaine na heroine na kwa ujumla kila kinachompelekea mtu kulewa.

Zipo hadithi nyingi za Mtukufu Mtume s.a.w. zinazokataza matumizi ya aina zote za vileo. Kwa mfano: Hadhrat Ibn Umar anasimulia kwamba Mtume s.a.w. amesema: Kila kinacholevya ni *khamr* (ulevi) na kila ulevi ni haramu. Yeyote atakayekuwa mnywaji wa ulevi duniani na akafariki katika hali hiyo bila ya kutubia basi hatopata kinywaji siku ya Kiama. (Muslim).

Endelea uk. 7

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashirat Rahman
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Simamisheni Sala kwa kuzingatia adabu zake

Kutoka uk. 1

na hali ya asili ya mwanadamu, hivyo itakuwa ni ngumu kulizungumzia jambo hili.

Hivyo Tanzeem zote na pia uongozi wa Jamaat unatakiwa kubuni mipango na taratibu ambazo kwa kadiri muda utakavyokuwa unaenda, mipango hiyo itapambana na uzembe na mapungufu na inatakiwa iwe na malengo ya kuleta maendeleo kila siku katika lengo hili la maisha ambalo Allah Mtukufu ndio ameifanya iwe ni sababu ya uwepo wetu. Maendeleo katika Ibada zetu ndio yatakayo tupatia ufaulu na jambo hili ni muhimu sana. Mfumo wote wa uongozi kwa ujumla unatakiwa kufanya kazi kwa bidii katika jambo hili. Lajna Imaillah wanatakiwa wahakikishe wanatimiza wajibu wao katika jambo hili. Wanatakiwa kuwa makini juu ya watoto zao wanapokuwa wanasali majumbani mwao na waifundishe tabia hii kwa watoto, vile vile kuhakikisha wanaume wa nyumbani mwao na kaka zao (ambao wapo majumbani) wanakwenda misikitini mara zote hili ni jukumu la Wanawake pia. Ikiwa wanawake watatimiza wajibu wao katika jambo hili, wataweza kuleta mabadiliko makubwa sana.

Vile vile ningependa kulizungumzia jambo hili kwa wale watu ambao wanasema wasikumbushwe katika sala zao au wanasema jambo hili la sala ni kati yao na Mungu Mtukufu. Wanawake wengi wanalalamika kuwa wakati wanapowakumbusha waume zao [kuhusu Sala] wanaanza kutoa hoja na mikwaruzano. Kwa watu hawa ninapenda kusema kuwa ijapokuwa jambo la sala ni kati ya mtu na Mola wake, lakini ni wajibu wa uongozi kuwakumbusha watu na kuweka msisitizo katika jambo hili. Kwa njia hiyo hiyo ni wajibu pia wa wake, na kwa hakika wajibu huo upo juu yao.

Ikiwa kama ilikuwa ni uamuzi wa mtu kwamba kama tu anataka anaweza kusali au kama anataka anaweza kuacha au ikiwa wakati wa sala ya Al-Fajr wanakuwa katika usingizi mkali na pia wanahitaji kufanya kazi siku nzima, hivyo wasiamshwe kwa ajili ya sala, ikiwa hii ndio hali yenyewe basi Mtukufu Mtume (s.a.w) asingeshauri mke na mume yeyote kati yao atakayekuwa wa kwanza kuamka, anatakiwa amuamshe mwenzake. Ikiwa haamki na bado anahisi usingizi, basi amnyunyuzie maji kidogo usoni mwake. Katika baadhi ya matukio Mtukufu Mtume (s.a.w) aliweka onyo madhubuti.

Katika hotuba iliyopita, nilieleza hadithi. Hivyo, ile fikra ya mtu kusema kwamba yupo huru kufanya anavyojisikia eti kwa kusema kwamba jambo hili ni kati yao na Mungu wao, hii sio sawa. Ikiwa kuna uongozi ambao mliufikiria wenyewe, ukumbushe juu ya hali za sala katika jamaat zenu, basi badala ya kuchukia na kukasirika mnatakiwa kuonyesha ushirikiano juu yao.

Ikiwa yupo mtu ambae anasali sala halafu anasimulia kwa wengine na anajisifu kwamba anasali sala ya jamaa mara zote, basi hilo ni jambo baya na sio sahihi. Hivyo, umuhimu wa sala unatakiwa ufahamike na kila mmoja wetu na juhudi kubwa zifanyike kwa ajili ya kufuata mafundisho ya Allah Mtukufu na Mtume wake (s.a.w).

Baada ya kuelezea haya, sasa nitaelezea baadhi ya mambo ya msingi kuhusiana na ibada ya sala kwa kutumia maneno ya Masih Aliyeahidiwa (a.s) ambayo kwa asili yamejaa falsafa na hekima, au ni mambo ambayo Masih Aliyeahidiwa (a.s) ametuwekea msisitizo juu ya hayo.

Mara nyingi watu wamekuwa wakiulizia mambo haya, hivyo ni muhimu kuyaelezea. Kwa fadhila za Allah, watu kutoka katika madhehebu mbalimbali ya Kiislam wanajiunga na Jumuiyya ya Islam ya Ahmadiyya. Na baadhi wanaendelea kushikilia baadhi ya tabia zilizopita ambazo hazitekelezwi na Jumuiyya ya Islam ya Ahmadiyya kwa sababu Masih Aliyeahidiwa (a.s) alishatutolea ufafanuzi wa mambo haya. Ikiwa tumempokea Masih Aliyeahidiwa (a.s) kama ni msuluhishi tunatakiwa kufuata mafundisho yake yote ambayo yanathibitisha yale matendo yaliyokuwa yanafanywa na Mtukufu Mtume (s.a.w) na Masahaba zake.

Miongoni wa mambo hayo, moja ni hili la Rafa' Yadain. Ambalo ni kuinua mikono yote miwili hadi kwenye ndewe za sikio baada ya kila Takbira [Yaani kusema Allahu Akbar (Mungu ni mkuu)] inapotamkwa, au baada ya kila tendo katika sala. Ni kwa sababu ya mambo haya madogo madogo ambayo tu sio yamesababisha mgawanyiko mkubwa au migawanyiko midogo miongoni wa Waislam, bali yamesababisha magomvi, ambayo dhehebu moja linaliita lingine kuwa ni makafiri. (Ikiwa mtu ameshiriki katika sala ya Jeneza iliyoongozwa na imamu wa dhehebu lingine, basi masheikh wanatangua ndoa ya mtu huyo na wanaivunja). Mambo haya sio mambo ya wakati uliopita, bali kwa hakika ni mambo yanayoibuka hata leo. Hivi karibuni kuna habari zimeeleza kuwa huko India kuna watu wa dhehebu fulani ambao walisali sala ya Jeneza nyuma ya mtu wa dhehebu lingine. Amri ilitolewa ya kufuta ndoa za wale wote walioshiriki. Wakazi wote wa kijiji hicho au mji huo walienda kwa Masheikh wao na kupanga msururu mrefu nje. Na ndoa zote zilifungwa upya. Watu hawa wanafanya dini kuwa ni kitu cha mzaha na wamesababisha kutokea kwa vurugu na machafuko.

Masih Aliyeahidiwa (a.s) ambae alitumwa ili kutatua migororo yote, alisema; "Mimi ni mshuluhishi, hivyo nipokeeni". Alileta ufumbuzi katika mambo ambayo yana utofauti mdogo na baadhi yao alitoa ruhusa ya kufanywa, alisema pia mtu anaweza kuchagua kufanya jambo kwa njia moja au nyingine. Kuhusiana na Rafa' Yadain [yaani kunyanyua mikono hadi kwenye ndewe za sikio] Masih Aliyeahidiwa (a.s) alisema; "Hakuna ubaya katika jambo hilo. Haina haja kwamba mtu ni lazima kulifanya au la, bali la zaidi ni kuwa mambo yote yameelezwa katika Hadithi. Pia jambo hili linaonekana zaidi katika matendo ya Wahhabi na Sunni, mmoja kati yao ameshikamana na Rafa' Yadai wakati mwingine hafanyi hivyo. Inaonekana mahali fulani kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w) alishika tendo hilo la Rafa' Yadain, lakini baadae aliliacha jambo hili. Halikuwa jambo lililodumu katika matendo ya Mtume mtukufu (s.a.w), ikiwa alilifanya jambo hilo sehemu fulani na baadhi ya watu wakashikamana nalo, basi linakubalika na hakuna haja ya kugombana katika jambo hili.

Ijapokuwa Masih Aliyeahidiwa (a.s) alikuwa anashikamana na matendo yale ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w) alishikamana nayo kwa muda mrefu. Kuhusu jambo hili kuna ushahidi mwingine ambao Hazrat Sahibzada Mirza Bashir Ahmad aliandika; "Hafiz Noor Muhammad Sahib, mkazi wa Faizullah Chak aliponiandikia barua alisema, kuna sehemu fulani tulimuuliza Masih Aliyeahidiwa (a.s) anafikiriaje juu ya swala la kusoma surat Fatiha nyuma ya Imam, Rafa' Yadain na kutamka Amin kwa sauti?. Masih Aliyeahidiwa (a.s) alisema; "Mambo haya yameelezwa katika Hadithi, hivyo mtu anaweza akayafanya".

Sahibzada Mirza Bashir Ahmad Sahib kuhusiana na jambo hili alisema: "Mtu anaweza akauliza kwa mapenzi kwamba kuhusiana na jambo la kusoma surat Fatihah pamoja na Imam, tendo hili linathibitika kufanywa na Masih Aliyeahidiwa (a.s) katika sehemu nyingi, yaani kusoma Surat Fatihah pamoja na Imam wakati wa sala ya Jamaa. Ijapokuwa kuhusiana na Rafa' Yadain na kutamka Amin Bil Jahr (kutamka Amin kwa sauti) siamini kwamba Masih Aliyeahidiwa (a.s) alilieleza jambo hili katika namna hiyo, kwa sababu kama Masih Aliyeahidiwa (a.s) angeliona jambo hilo kuwa ni sahihi, angekuwa analitekeleza au angekuwa analifanya mara moja moja, bali katika matendo ya Masih Aliyeahidiwa (a.s) tunaona kinyume chake. Ni imani yangu kwamba Hafiz Sahib alipokuwa amemuuliza Masih Aliyeahidiwa (a.s), kwa sababu swali lake lilikuwa na vipengele vingi, basi Masih Aliyeahidiwa (a.s) alielezea kipengele cha kwanza tu cha swali hilo, yaani jibu la Masih Aliyeahidiwa (a.s) alielezea tu katika upande wa kusoma surat Fatihah pamoja na Imam, vinginevyo Allah anajua zaidi".

Kuna simulizi nyingine ambayo inathibitisha kuwa kusoma surat Fatihah pamoja na Imam kumeruhusiwa, lakini sio zaidi ya hilo. Sahibzada Mirza Bashir Ahmad anaandika: "Mian Abdullah Sanori Sahib aliniambia kwamba: "Hapo mwanzo nilikuwa nachukia kabisa kufuata fiqih au sunna yoyote, na nilikuwa nimeshikilia kwa uthabiti mkubwa desturi ya Rafa' Yadain na Amin Bil Jahr yaani kutamka Amin kwa sauti kubwa. Hata baada ya kukutana na Masihi Aliyeahidiwa (a.s) niliendelea na desturi hii kwa miaka mingi. Baada ya muda fulani nilipata nafasi ya kusali nyuma ya Masih Aliyeahidiwa (a.s). Sala ilipomalizika Masih Aliyeahidiwa (a.s) alinigeukia na alitabasamu na kisha akasema: "Mian Abdullah, umeendelea na desturi hii kwa muda mrefu vya kutosha." Akitaja juu ya Rafa' Yadain yaani kunyanyua mikono yote hadi kwenye ndewe za sikio baada ya kila Takbira.

Mian Abdullah Sahib aliendelea kwa kusema: "Kuanzia siku hiyo nikaachana na desturi ya Rafa' Yadain, na pia nikaacha kutamka Amin Bil Jahr (yaani kutamka Amin kwa sauti kubwa)." Mian Abdullah Sahib alisema, "sikuwahi kumuona Masih Aliyeahidiwa (a.s) akiwa na desturi ya kufanya tendo la Rafa' Yadain au kumsikia akisema Amin Bil jahr, au kumsikia akitamka Bismillah (yaani kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, mwingi wa Ukarimu) kwa Sauti." Mirza Bashir Ahmad Sahib alisema: "Hizi ni njia ambazo mtu anazikubali, kwamba ndio desturi za Masih Aliyeahidiwa (a.s) ambazo ndio sahihi kama zilivyoelezwa na Mian Abdullah Sahib na kuthibitishwa, ijapokuwa matendo yetu kama Waahmadiyya tangu zama za Masih Aliyeahidiwa (a.s) na hata baada yake, hadi hivi leo hakuna mtu anayeleta lawama dhidi ya wengine.

Baadhi hutamka Amin kwa sauti, wakati wapo wengine ambao hawatamki, na wapo baadhi walio na destuti ya kufanya Rafa' Yadain, lakini wengi wao huwa wanaacha mambo hayo na kwa hakika hayatekelezwi sasa, isipokuwa kwa wale ambao wamejiunga na jamaat hivi karibuni na walikuwa na desturi ya kufanya hivyo, lakini hata wao pia taratibu taratibu wanaachana na desturi hiyo." Akaendelea kusema, "Baadhi ya watu wanatamka Bismillah kwa sauti, lakini wengi wao hawafanyi hivyo. Masih Aliyeahidiwa (a.s) alisema kiuhalisia njia zote hizi zinaonekana katika matendo ya Mtukufu Mtume (s.a.w), ingawa ile desturi ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w) alishikamana nayo katika sehemu mbalimbali hiyo ndio njia sahihi, na Hiyo ndio ilikuwa desturi ya Huzur (a.s) [yaani Masih Aliyeahidiwa(a.s)].

Kisha kuna swali linasema kwamba wakati wa Sala, katika kipindi cha Qiyam [yaani kusimama wima katika sala] wakati mtu anapofunga mikono yake, Je ni sehemu gani ambayo mtu anatakiwa kukunja mikono yake? Sahibzada Mirza Bashir Ahmad sahib anaandika. "Katika sehemu fulani Maulvi Sarwar Shah Sahib aliniambia, 'wakati Hazrat Khalifatul Masih I (ra) alipopokea barua fulani, kuwa kuna baadhi ya watu wanafunga mikono yao chini ya kitovu, baadhi katikati na baadhi wanafunga mikono juu zaidi. Hazrat Khalifatul Masih I (r.a) alipokea barua hiyo iliyosema ikiwa mtu ameweka nia ya kusali sala, Je ni mahala gani anatakiwa afunge mikono yake?.

Katika barua iliandikwa kuwa, Je ipo hadithi sahihi iliyoandikwa kwamba mtu afunge mikono yake juu ya kitovu? Hazrat Khalifatul Masih I (r.a) aliifikisha barua hiyo kwa Masih Aliyeahidiwa (a.s) na alisema, 'hadithi zinazohusiana na jambo hili nyingi zina mabishano na kuna majadiliano mengi kuzihusu hizo. Baadhi ya watu wanasema zipo sahihi na baadhi wanasema kuwa haziko sahihi'. Masih Aliyeahidiwa (a.s) alisema; " Maulvi Sahib! Ukilifuatilia jambo hili utagundua kitu fulani, (Masih Aliyeahidiwa (a.s) akijizungumzia yeye mwenyewe) katika miaka yangu ya mwanzo, ijapokuwa kila mtu aliyekuwa amenizunguka alikuwa anafuata Fiqih ya Wahanafi, mimi sikupenda kamwe kufunga mikono yangu chini ya kitovu wakati wa sala, kinyume chake nilikuwa napenda kufunga mikono yangu juu ya eneo la kitovu na tumeyafanya hayo katika matukio mengi.

Masih Aliyeahidiwa (a.s) alisema:

Nina uzoefu katika matukio mengi kwamba ninapokuwa ninafanya jambo fulani kama desturi, basi ninapolifanyia utafiti, nimekuwa napata uthibitisho mara kwa mara ukiongozana na hadithi pia. "Masih Aliyeahidiwa (a.s) akaendelea kusema zaidi, 'hata kipindi ninapokuwa sina ufahamu wa kutosho kuhusu jambo hilo (yaani la Hadithi)'

Hivyo, Masih Aliyeahidiwa (a.s) alimwambia Hazrat Khalifatul Masih I (r.a) kwamba 'litafute jambo hilo na utafanikiwa kuliona, kwa sababu mara nyingi huwa ninaona kwamba kama katika hali ya asili nitakuwa ninalielekea jambo fulani kama desturi, basi pia huwa ninapata hadithi inayoniunga mkono juu ya jambo hilo'

Maulvi Sarwar Shah Sahib anasimulia kwamba 'sawa na Maagizo haya, Hazrat Khalifatul Masih I (r.a) aliondoka na mnamo dakika 30 hivi tangu aondoke, alirudi akiwa mwenye furaha sana huku akiwa ameshika kitabu mkononi mwake. Akamtaarifu Masih Aliyeahidiwa (a.s) kwamba ameiona hadithi na kwa hakika hadithi alioiona ipo kwenye mamlaka ya Hazrat Abu Bakar (r.a) na Hazrat Umar (r.a) na hivyo haiwezi kupingwa au kutiliwa shaka. Akaendelea kusema zaidi hii yote ni kwa sababu ya baraka ya maelekezo ya Huzur, na ndio maana alifanikiwa kuipata hadithi inayosema kufunga mikono juu ya kitovu ndio ilikuwa desturi ya kudumu ya Mtukufu Mtume (s.a.w).

Hazrat Hajji Ghulam Ahmad anasimulia kwaba, 'mtu mmoja

Endelea uk. 4

Simamisheni Sala kwa kuzingatia adabu zake

Kutoka uk. 3

alitatizwa na sehemu gani haswa ambayo mtu anatakiwa kufunga mikono yake wakati wa sala'

Baadhi ya watu wanajifungia mipaka katika mambo yenye utata. Kwa upande mwingine Masih Aliyeahidiwa (a.s) alitoa maelekezo ya kutafuta hadithi na akasema kwa hakika itapatikana kwa sababu hali yake ya asili ilikuwa inamfanya awe anafunga mikono juu ya kitovu. Ijapokuwa, kwa upande mwingine kuna mtu mwingine alikuwa anatatizwa na jambo hilo hilo, lakini katika hili mabadiliko kwake yalikuwa ni jambo la lazima kuhusu uelewa wake mbaya. Hivyo Masih Aliyeahidiwa(a.s) alipomjibu alisema:

'Vitendo vya kidhahiri vya heshima pia vina umuhimu mkubwa na kwa hiyo vitendo vya mwili katika sala pia ni vya muhimu, hata hivyo msisitizo mkuu wa mtu katika sala lazima uwe kujielekeza kwa Mungu.' Ingawa vitendo vya kimwili pia ni vya muhimu lakini mtu ni lazima pia aelekeze fikra zake kwa Mungu Mwenyezi Ambaye ndiye lengo la msingi la sala.

Swali liliulizwa kuhusu kunyanyua kidole wakati wa kusoma Tashshahud (kutangaza imani). Mtu mmoja aliuliza kwamba kwa nini kidole cha shahada kinainuliwa wakati wa kusoma Atahiyyat [dua inayosomwa wakati wa jilsa]? Masihi Aliyeahidiwa (as) alijibu: Katika zama za kabla ya Islamu, watu walikuwa wakinyanyua kidole hiki kama alama ya kuonyesha kutukana na maneno machafu. Hivyo, kilikuwa kinaitwa kidole cha Sabaaba [tusi]. Allah Mwenyezi Aliwarekebisha watu wa Uarabuni na Akaondoa tabia hii na badala yake Akawaambia kunyanyua kidole hiki ili kushuhudia Umoja wa Mungu. Na kwa hiyo, kidole hicho hakitajulikana tena kama kidole cha kutukania, bali kitajulikana kuwa kidole kinachoshuhudia umoja wa Mungu'.

Masihi Aliyeahidiwa (as) alielezea zaidi:

'Halikadhalika, Waarabu walikuwa wakinywa pombe mara tano kwa siku, lakini badala yake Allah Mwenyezi Amewawekea sala tano kwa siku nzima.

Swali liliulizwa kuhusu kusoma dua zilizomo ndani ya Qur'an wakati wa Ruku (kuinama) na Sujudu. Maulvi Abdul Qadir Sahib Ludhianvi aliuliza kama ilikuwa inaruhusiwa kusoma dua zilizomo ndani ya Qur'an wakati wa Rukuu na Sujuud. Masihi Aliyeahidiwa (as) alijibu:

'Sajda na Ruku zinaonyesha hali za unyenyekevu wa hali ya juu na upole, hata hivyo Neno la Allah linahitaji heshima kubwa na utukufu, lakini mbali na hili haijawahi kuandikwa popote katika Ahadith kwamba Mtume Mtukufu (saw) alikuwa akisoma dua zilizomo ndani ya Qur'an alipokuwa katika Sajda au Ruku'

Hazrat Sahibzada Mirza Bashir Ahmad Sahib anasema kuhusiana na Mia Khairuddin Sahib Sikhwani alimueleza kwenye barua kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema:

'Mtu ni lazima aombe sana katika sala na maombi ni lazima yafanywe kwa lugha yake mwenyewe lakini yale maneno ambayo yamewekwa na suna ya mwenyewe Mtume Mtukufu (saw) ni lazima yasomwe kwa namna hiyo hiyo. Kwa mfano, kusoma Subhana Raabi Al-Adhiim [Mtukufu Mola wangu, Mkuu kuliko wote] wakati ukiwa kwenye Rukuu na kusoma Subhana Raabi Al-Aa'la [Mtukufu Mola wangu, Yu juu kuliko wote] wakati wa Sajda, na baadae mtu anaweza kuomba kwa lugha yake.'

Masihi Aliyeahidiwa (as) aliendelea kuelezea zaidi:

'Dua zilizomo ndani ya Qur'an zisisomwe wakati wa Rukuu na Sajda kwa sababu Qur'an Tukufu ni Neno halisi la Allah Mwenyezi na ni lenye utukufu mwingi wakati hali ya Sajda inaonyesha hali ya unyenyekevu kamili, kwa hiyo mtu aione Qur'an Tukufu ni yenye heshima kubwa.

Mtu mmoja alimuuliza Hazrat Khalifatul Masih II (ra) kwamba kwa nini inakatazwa kusoma dua zilizomo ndani ya Qur'an wakati wa Sajda wakati kwa kweli Sajda inaakisi hali ya unyenyekevu kamili na kwa hiyo dua zingekubaliwa haraka zaidi kama zingesomwa katika hali ya Sajda? Hazrat Khalifatul Masih II (ra) alijibu:

'Mimi pia nilikuwa naona kwamba ilikuwa inaruhusiwa kusoma dua zilizomo ndani ya Qur'an wakati wa Sajda mpaka nilipokutana na nukuu ya Masihi Aliyeahidiwa (as) ambamo alikataza kusoma dua zilizomo ndani ya Qur'an wakati wa Sajda na kuna Hadithi kwenye Musnad Ahmad bin Hanmbal ambayo pia inaunga mkono hili.

Hazrat Khalifatul Masih II (ra) anelezea zaidi kwamba:

'Hata kama nisingekutana na nukuu zinazopinga mtizamo wangu wa kwanza, hata hivyo bado nisingeziona hoja zilizotolewa kuwa muafaka; ambamo alisema kwamba kwa kuwa Sajda ni hali ya unyenyekevu wa hali ya juu kwa hiyo kusoma dua zilizomo ndani ya Qur'an lazima kuruhusiwe. Hii sio hoja.'

Hazrat Khalifatul Masih II (ra) wakati akifafanua zaidi kuhusu hili alitoa mfano wa imani inayoshikwa na Imam Malik na akasema:

'Kila kitu kinachoishi ndani ya maji ni Halal. Siku moja, mtu fulani alimuuliza (Imam Malik) kwamba nguruwe pia anaishi majini, kwa hiyo anaruhusiwa kuliwa? Imam Malik alijibu kwamba kila kitu kinachoishi ndani ya maji ni Halal lakini nguruwe ni Haram. Hata hivyo aliendelea kuuliza swali hilo lakini Imam Malik alijibu kwamba ninaweza kusema tu kwamba kila kitu kinachoishi ndani ya maji ni Halal lakini nguruwe ni Haram.

Hazrat Khalifatul Masih II (ra) anaelezea zaidi:

'Nitatoa jibu kama hilo kwa swali hili ambalo ni kwamba naam Sajda ina akisi hali ya unyenyekevu wa hali ya juu lakini dua zilizomo ndani ya Qur'an haziwezi kusomwa katika hali hii. Dua zinamfanya mtu awe mpole wakati Qur'an Tukufu inamnyanyua mtu na kwa hiyo imekatazwa kusoma dua zilizomo kwenye Qur'an wakati wa Sajda. Pale tunapoona desturi inayoweza kusemwa kuwa ni ya Mtume Mtukufu (saw) na Masihi Aliyeahidiwa (as) basi hairuhusiwi kwetu kuanzisha desturi inayopingana na hiyo hata kama hatuielewi kikamilifu. Jukumu letu ni kuyashika maagizo tu.'

Baadhi ya watu wanauliza kwamba kama wakijiunga na sala wakati wa Ruku, je hiyo bado inahesabiwa kuwa ni Rakaa. Kwa ujumla, kila mmoja wetu anajua hili na wanaambiwa hili tokea utotoni kwamba kama mtu amewasili akiwa amechelewa kwenye sala na amejiunga wakati wa Rukuu basi hiyo inahesabiwa kuwa ni Rakaa. Siku moja swala hili la kama Rakaa ya mtu wa aina hiyo inahesabiwa ambaye amejiunga wakati wa Rukuu tu lililetwa na Masihi Aliyeahidiwa (as) aliomba maoni ya wasomi wengine waliokuwepo. Uamuzi wa madhehebu mengine katika Islam pia yalipatikana. Mwishoni, Masihi Aliyeahidiwa (as) alitoa hukumu yake na akasema:

'Imani yetu ni …….. (maneno ya kiarabu) yaani bila ya Surah Al-Fatiha hakuna Salat. Iwe mtu anaongoza sala au anasali peke yake, ni lazima wasome Surah Al-Fatiha. Hata hivyo, waisome taratibu ili maamuma waweze kuisikia na pia kuisoma wao wenyewe (hapa Masihi Aliyeahidiwa (as) anatoa maagizo kwa Imamu anayeongoza sala). Au, baada ya kila aya, Imam atoe muda wa kutosha ili maamuma waweze pia kuisoma. Kwa hali yoyote ile, maamuma ni lazima wapewe fursa ya kusikiliza usomaji na pia kuisoma wao wenyewe. Usomaji wa Sura Al-Fatiha ni wa muhimu kwa sababu ni Ummul Kitaab yaani Mama wa Kitabu, lakini hata hivyo pamoja na jitihada za hali ya juu za mtu kujiunga na sala lakini ameweza kujiunga tu wakati wa Rukuu na amekosa sehemu ya mwanzo ya sala, bado itahesabiwa kuwa ni Rakaa kwake. Ingawa hakuweza kusoma Surah Al-Fatiha, hata hivyo imetajwa katika Ahadithi kwamba yeyote anayejiunga na sala wakati wa Rukuu, Rakaa yake inahesabiwa.

Masihi Aliyeahidiwa (AS) anaelezea zaidi:

'Kuna vitu viwili kuhusiana na mambo ya aina hiyo. Kwa upande mmoja, Mtume Mtukufu (saw) alitamka na akasisitiza sana kuisoma Surah Al-Fatiha katika sala na kwamba ni Ummul Kitaab [Mama wa kitabu] na ni maana hasa ya sala. Hata hivyo, kama mtu pamoja na jitihada yake yote ameweza kujiunga na sala wakati wa Rukuu, basi kwa kuwa msingi wa Islam uko katika kuleta wepesi hivyo Mtume Mtukufu (saw) alitamka kwamba bado itahesabiwa kuwa ni Rakaa. Haikutajwa Surah Al-Fatiha, kwa kweli katika hali kama hiyo, mtu atashikilia msamaha ulio ruhusiwa kutokana na kuwasili akichelewa katika sala'.

Masihi Aliyeahidiwa (AS) anaelezea zaidi:

'Allah Mwenyezi Ameifanya hali ya moyo wangu kwa namna ambayo moyo wangu unatetemeka ukiona sura ya kitu kilichokatazwa na moyo wangu unanigeuzia mbali katika kufanya kitendo cha namna hiyo. Kuna ushahidi wa wazi kwamba kama mtu anamaliza sehemu tatu za sala lakini kutokana na vipingamizi nje ya uwezo wake anamalizia sehemu nyingine nusunusu basi hakuna shida. Katika hali kama hiyo mtu aridhike na msamaha ulioruhusiwa. Lakini, mtu ambaye kwa makusudi anaonyesha uvivu na anajiunga na sala akichelewa, basi sala ya mtu huyo yenyewe inakuwa batili.

Zaidi ya hayo, kuhusiana na kumfuatisha Imam katika kuisoma Surah Al-Fatiha, Hazrat Mirza Bashir Ahmad anaandika:

'Maulvi Sher Ali Sahib ameniambia kwamba Masihi Aliyeahidiwa (AS) alikuwa akiwakazania maamuma kumfuatisha Imamu katika kuisoma Sura Al-Fatiha. Hata hivyo, pamoja na hili, alikuwa akitamka pia, 'ingawa ninaamini kwamba Surah Al-Fatiha ni ya muhimu lakini sisemi kwamba sala ya mtu haiwi sawa ambaye hasomi Surah Al-Fatiha kwa sababu kumekuwa na watakatifu wengi na wenye hekima zamani ambao hawakuona usomaji wa Surah Al-Fatiha kuwa ni wa muhimu na siwezi kuamini kwamba sala zao hazikuwa sawa.'

Hazrat Mirza Bashir Ahmad anaendelea kuandika:

'Huyu mpole anatamka kwamba Hanafi wanaitakidi kwamba maamuma wasimame kimya nyuma ya Imam na ni lazima wasikilize usomaji wake na wasisome chochote wao wenyewe. Watu wa Ahle Hadith hata hivyo wanaamini kwamba maamuma ni lazima pia wamfuatishe Imam katika kusoma Sura Al-Fatiha. Masihi Aliyeahidiwa (AS) alikuwa anaunga mkono msimamo wa Ahli Hadith lakini pamoja na hili hakukubaliana na maoni ya Ahli Hadith kwamba sala ya mtu haiwi sawa kama Sura Al-Fatiha haisomwi.

Akijibu swali ambalo liliulizwa na Munshi Rustam Ali Sahib, Masihi Aliyeahidiwa (AS) aliandika:

'Sala ya maamuma itakuwa imekamilika kama hawatarudia kuisoma Sura Al-Fatiha, hata hivyo ni vyema kuisoma. Kama Imam anaisoma kwa haraka haraka, basi mtu aisome polepole hata akisoma aya moja au mbili. Kama Imam anasoma kwa haraka haraka na maamuma wanaweza kusoma aya moja au mbili katika muda huo basi wasome chochote wanachoweza lakini sio kwa namna yenyewe itakayowazuia kusikiliza anachosoma Imam. Kama mtu hawezi kuirudia basi hilo ni jambo ambalo liko nje ya uwezo wake lakini bila kuangalia hilo mtu ni lazima asikilize usomaji wa Qur'an wa Imamu na hiyo itatosheleza lakini bila shaka haitakuwa sala ya daraja ya juu.

Hazrat Mirza Bashir Ahmad anaandika kwamba Mia Khairuddin Sahib Sikhwani alimuambia kwenye barua kwamba siku moja nilimuuliza Masihi Aliyeahidiwa (as) kuhusiana na kumfuatisha Imamu katika usomaji wa Surah Al-Fatiha. Masihi Aliyeahidiwa (as) akajibu, 'ni vyema kumfuatisha Imam katika usomaji wa Surah Al-Fatiha.' Kisha nikauliza kwamba sala inaswihi kama mtu hawezi kumfuatisha Imamu. Masihi Aliyeahidiwa (as) akajibu,' sala inaswihi lakini ni vyema kumfuatisha Imamu katika usomaji wa Surah Al-Fatiha.' Masihi Aliyeahidiwa (as) alielezea zaidi, 'kama sala ingechukuliwa kwamba haiswihi kutokana na kutomfuatisha Imamu katika usomaji wa Surah Al-Fatiha sasa ingewezekanaje wale watawa wote wachaMungu wa dhehebu la Hanafi kupata daraja za juu kiasi kile cha uchaMungu? Watakatifu wengi kutoka zamani hawakusoma Surah Al-Fatiha na hawakuwa wanaunga mkono kuirudia.'

Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza zaidi, 'Sala inaweza kuswaliwa katika namna zote mbili, lakini hata hivyo tofauti ni kwamba ni namna ipi ambayo ni kubwa zaidi. Kwa njia hiyo hiyo kusema 'Amiin' kwa sauti ndogo kunapendelewa zaidi ya kuisema katika sauti kubwa'

Pir Siraj-ul-Haq anasimulia kwamba Hazrat Maulvi Abdul Karim Sahib alikuwa akisema kwamba mtu mmoja alikuwa akiishi Sialkot au karibu na eneo hilo. Kila siku tulikuwa tukimuambia amfuatishe Imam katika usomaji wa Sura Al-Fatiha na tulitoa kila hoja iliyowezekana kumshawishi lakini alishindwa kusikiliza na alikuwa akisali pamoja nasi lakini bila kumfuatisha Imamu katika usomaji wa Sura Al-Fatiha. Siku moja, alikwenda kumtembelea Masihi Aliyeahidiwa (as) huko Qadian na mazungumzo yalizuka kuhusiana na suala hili. Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba Sura Al-Fatiha irudiwe baada ya Imamu na hakutoa hoja yoyote kutoka kwenye Qur'an Tukufu wala Hadithi kuthibitisha hili. Hata hivyo, mtu huyu aliposikia hivi alianza kumfuatisha Imamu katika usomaji wa Sura Al-Fatiha bila ya mjadala wowote.

Mtu mmoja alimuuliza Masihi Aliyeahidiwa (as) kwamba sala ya mtu inakubaliwa kama hatasoma Alhamdulillah baada ya Imamu? Masihi Aliyeahidiwa (as) alijibu:

'Swali lisiwe kwamba sala itakubaliwa au hapana. Bali unachotakiwa kuuliza ni kama mtu asome Alhamdullillah nyuma ya Imamu au hapana. Ninasema kwamba hakika ni lazima isomwe. Allah Mwenyezi pekee Anajua kama sala inakubaliwa au vinginevyo. Wale wanaofuata

Endelea uk. 5

Simamisheni Sala kwa kuzingatia adabu zake

Kutoka uk. 4

madhehebu ya Hanafi hawaisomi. Maelfu ya Auliyah (marafiki wa Allah) zamani walifuata njia ya Hanafi na hawakuisoma Alhamdullillah nyuma ya Imamu. Tunawezaje kuwaita Auliyah kama sala zao zilikataliwa? Kwa njia moja tunafanana na Imamu Adhama (Imamu Abu Hanifah) na tunamheshimu sana. Hatuwezi kutoa Fatwah kuhusiana na kupokelewa kwa sala yoyote. Katika zama hizo, hadithi zote zilikuwa bado hazijakusanywa na walikuwa hawajui uhakika wa suala hili ambalo sasa liko bayana. Hivyo, walisamehewa lakini leo suala hili limetatuliwa na sasa kama mtu haisomi, basi sala yake kwa hakika haitafikia hadhi ya kukubaliwa. Jibu langu mara zote kwa swali hili daima litakuwa kwamba Alhamdullillah ni lazima isomwe nyuma ya Imamu.'

'Siku moja nilimuuliza Masihi Aliyeahidiwa (as) kwamba ni wakati gani mtu arudie Alhamdulillah, ambapo alijibu: 'Uisome kila unapopata fursa.' Niliuliza: 'je iwe katika zile nyakati Imamu ananyamaza katika usomaji wake?' Masihi Aliyeahidiwa (as) alijibu: 'Wakati wowote fursa inapopatikana bila shaka ni lazima isomwe.'

Wakati fulani kuhusiana na mfuatano wa sala wakati zinachanganywa, mtu anayefika amechelewa anaweza asiwe na uhakika kamili ni sala ipi inayosaliwa, mfano Zuhr na Asr au Maghrib na Ishaa. Hazrat Khalifatul Masih II (ra) alisema: 'Mimi mwenyewe nilimsikia Masihi Aliyeahidiwa (as) akisema kwamba kama mtu ameingia katika msikiti wakati akiwa hajasali sala ya Adhuhuri, lakini sala ya Alasiri inaendelea, basi ni lazima kwanza asali sala ya Adhuhuri peke yake na kisha ajiunge na Imamu. Kama mtu anaingia msikitini wakati hajasali sala ya Magharibi lakini sala ya Isha inasaliwa, basi ni lazima kwanza asali sala ya Maghrib peke yake kisha baadae ajiunge na Imamu.

Kwa sala ambazo zinaunganishwa, kama mtu ameingia msikitini akiwa amechelewa wakati sala tayari zimeisha anza Masihi Aliyeahidiwa (as) ametoa Fatwa kwamba kama akitambua kwamba Imamu anasalisha sala ya Alasiri, basi kwanza asali sala ya Adhuhuri peke yake na kisha ajiunge na Imamu. Halikadhalika, kama mtu akijua kwamba Imamu anasalisha sala ya Ishaa, basi kwanza asali sala ya Magharibi peke yake kisha ndio ajiunge na Imamu. Lakini, kama mtu anakuwa hawezi kutambua ni sala ipi inayosalishwa, basi hapo ajiunge tu na jamaa. Katika hali kama hiyo, sala Imamu anayoongoza inakuwa ndio sala anayoisali. Baadae, asali sala ya kabla. Kwa mfano, sala ya Isha inasaliwa na mtu anaingia ambaye hajasali sala yake ya Magharibi. Kama atajua kwamba ni Isha inayosaliwa ni lazima kwanza asali sala yake ya Magharibi peke yake na kisha ajiunge na Imamu mara atakapomaliza. Lakini kama hajui ni Sala ipi inayosaliwa, basi ajiunge tu na Imamu katika sala. Katika hali hii sala yake ya Ishaa inakuwa imekamilika na asali sala yake ya Magharibi baadae. Hivyo hivyo itakuwa kwa sala ya Alasiri.

Masihi Aliyeahidiwa (as) kisha aliulizwa: Hairuhusiwi kusali sala yoyote baada ya Asr. Hivyo, kama mtu bila kujua anajiunga na sala ya Alasiri, anawezaje kuruhusiwa kusali sala ya Adhuhuri baadae? Masihi Aliyeahidiwa (as) alijibu: 'Ni sahihi kwamba kisheria sala haziruhusiwi baada ya sala ya Alasiri. Lakini, hii haiwezi kuchukuliwa kumaanisha kwamba mtu hawezi kusali sala ya Adhuhuri hata kama hali itatokea kwa bahati mbaya au kwa kughafilika. Katika hali za namna hii mtu anaruhusiwa kusali sala ya Adhuhuri baada ya sala ya Alasiri. Kama mtu hakuwa anajua [kuwa Asr inasaliwa] basi inaruhusiwa kusali Zuhr baadae, lakini kama mtu alikuwa anajua kuwa hiyo ndio hali [kwamba Asr ilikuwa inasaliwa] hapo hairuhusiwi.'

Anasema: 'Mimi mwenyewe nimemsikia Masihi Aliyeahidiwa (as) akifafanua swala hili sio mara moja tu, bali mara mbili. Ninakumbuka kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) aliulizwa kuhusu suala hili tena na akajibu: 'Nimekwisha eleza suala hili hapo kabla kwamba mpangilio wa mfuatano wa sala ni wa muhimu. Lakini, kama mtu hawezi kujua ni sAla ipi inayosalishwa na Imamu, kama ni Asr au Ishaa, basi ajiunge tu na Imamu. Sala inayosalishwa na Imamu itahesabiwa kuwa ndio sala anayosali yule anayejiunga. Baada ya hapo mtu huyo peke yake asali sala ya kabla.'

Ilikuwa ni desturi ya Masihi Aliyeahidiwa (as) kusali sala za Sunna nyumbani kabla na baada ya Sala. Hazrat Yaqub Ali Irfani Sahib anaandika kwamba tokea mwanzoni ilikuwa ni desturi ya Masihi Aliyeahidiwa (as) kusali sala zake za Sunna na Nawaafil nyumbani na alikuwa akisali sala za fardh kwa Jamaa msikitini. Aliendelea na desturi hiyo hadi mwisho. Lakini, baadhi ya siku alipoona watu wamejiunga na sala za Jamaa nyuma yake na hawajazimaliza, alikuwa akisali sala zake za Sunna msikitini kwa sababu njia ya kutokea ilizibwa kutokea nyuma. Katika nyakati zingine wakati Masihi Aliyeahidiwa (as) alipobakia msikitini baada ya sala zake, alikuwa akisali sala zake za Sunna msikitini. Kwa kuwa hii ilikuwa ni desturi ya Masihi Aliyeahidiwa (as). Baadhi ya wanafunzi/ waulizaji wajinga walianza kufikiri kwamba pengine kusali Sunna sio jambo la lazima, kwa sababu hawajawahi kumuona Masihi Aliyeahidiwa (as) akizisali aidha kabla au baada ya sala. Hazrat Khalifatul Masih I (ra) siku moja alilizungumzia hili katika Darsul Kuran (mafunzo rasmi ya Qur'an) yake na akasema: 'Ilikuwa ni desturi ya Masihi Aliyeahidiwa (as) kwamba mara baada ya kusali sala ya Faradhi alikuwa akienda nyumbani kwake.

Matokeo yake, watoto wengi wasio na busara walianza tabia ya kuondoka msikitini mara baada ya sala ya Faradh na ninaamini kwamba hawasali Sunna (nimeona kwamba hili linatokea mara kwa mara hata leo hii). Ni lazima watambue kwamba kitu cha kwanza Masihi Aliyeahidiwa (as) alichokifanya alipofika nyumbani ni kusali Sunna. Mimi pia ninafuata desturi hii.' Hazrat Khalifatul Masih I (ra) kisha akauliza: 'Kuna yeyote hapa ambaye anaweza kutoa ushahidi kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) alikuwa na desturi hii ya kusali Sunna mara tu afikapo nyumbani?'

Hapo Hazrat Mirza Bashir-ud-din Mahmud Ahmad (ra), ambaye kama kawaida alikuwepo kwenye Darsa, alitamka kwa sauti kubwa: Bila shaka yoyote, daima ilikuwa ni desturi ya Masihi Aliyeahidiwa (as) kusali sala za Sunna nyumbani kabla hajaenda msikitini, kisha alikuwa akisali sala za fardh msikitini, na kisha alirudi nyumbani na kusali sala zake za Sunna kabla ya kufanya chochote. Alikuwa akifanya kazi zingine pale tu alipomaliza kusali sala zake za Sunna.' Baada ya hili Hazrat Sahibzada Mirza Bashir Ahmad [mtoto wa Masihi Aliyeahidiwa (as)] pia alitoa ushahidi wake kuthibitisha hili. Baadae Hazrat Mir Nasir Nawwab Sahib, Hazrat Sahibzada Mir Muhammad Ishaaq Sahib na kisha pia mfanyakazi mzee wa Masihi Aliyeahidiwa (as), Hafiz Hamid Ali Sahib, wote walitoa ushahidi wao wa kuona.

Mtu mmoja alimuuliza Masihi Aliyeahidiwa (as) kama mtu auchukue Uimamu (kuongoza sala) kuwa ndio kazi yake ya ajira. Katika baadhi ya sehemu, kuna mashekhe wanaoongoza sala kwa ajili tu ya kupata fedha. Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema:

'Nitapata wasiwasi wa kujiunga na sala nyuma ya mtu ambaye anauchukua uimamu kuwa ajira. Itafahamika na watu wote kwamba mtu huyo ameuchukua uimamu kuwa ndio kazi yake. Hivyo, kwa kweli haendi kuongoza sala mara tano kwa siku, bali anaendesha duka ambalo analifungua katika nyakati hizo. Familia yake na watoto wanategemea kwa ajili ya maisha kilichopatikana katika duka hili. Matokeo yake, watu wanafikia hatua ya kupeleka kesi zao mahakamani kupinga uteuzi au kufukuzwa kutoka kwenye nafasi hizo [za uimamu]. Ili kulazimisha washinde kesi za uimamu mashekhe hawa huwa wanakata rufaa baada ya rufaa. Kwa kifupi huu sio uimamu, bali hii ni njia iliyokatazwa ya kujipatia fedha kwa namna isiyofaa.'

Kesi zinafunguliwa na wale wanaong'ang'ania kuwa maimamu wenyewe katika eneo fulani. Kisha migogoro mirefu inaibuka na hili linaendelea hata leo. Zaidi akielezea kama inafaa kufuata katika sala nyuma ya ambaye anasalisha kama ajira, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema:

'Kwa maoni yangu haifai kusali sala nyuma ya mtu anayefanya hivyo kwa ajili ya maisha. Wanaongoza sala kwa sababu tu ya kupata mishahara yao ya kila wiki na mkate. Wataacha kama hawatapata hayo. Kama maisha yanapatikana kwa nia za kiuchaMungu, inakuwa ni aina ya ibada. Kama mtu anawajibika katika kazi yake kwa kujituma na kidhati hajisikii kupata shida au kubebeshwa mzigo na kazi hiyo, bali inakuwa ni kitu rahisi kwake kukifanya.

Kuhusiana na kusali nyuma ya wale wanamuita Masihi Aliyeahidiwa (as) muongo na kafiri, Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema:

'Ni kosa kabisa na Haraam. Wale wanaoniita mimi kuwa niko nje ya Islam na kuwa ni muongo, hao ni watu walioangamia na kuhilikishwa. Kwa hiyo, haimpasi yeyote kutoka katika Jumuiya yangu kusali nyuma ya watu wa aina hiyo. Mtu hai anaweza kusali nyuma ya mfu? Kumbukeni kwamba Allah Mwenyezi Amenifahamisha kuwa imekatazwa kabisa kusali nyuma ya ambaye ananiita mimi muongo na mzushi. Bali Imamu wenu ni lazima awe ni miongoni mwenu. Hii imeonyeshwa katika Hadithi ya Bukhari inayosema: Imamu kum min kum: Imamu wenu atatokana miongoni mwenu.'

Kisha kuhusiana na sababu ya kutokusali nyuma ya Waislamu wasio kuwa Waahmadiyya, mtu mmoja alimuuliza Masihi Aliyeahidiwa (as) kwamba kwa nini inakatazwa kusali nyuma ya wale ambao sio wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema:

'Watu hao wameachana na Taqwa ambao wanadhana mbaya, haraka wanaikataa jumuiya hii iliyoanzishwa na Allah Mwenyezi na wanazipuuza ishara nyingi zisizohesabika na hawajali majanga yanayoikuta Islam. Neno la Allah [Qur'an Tukufu] linasema kwamba "Allah Anawakubalia wachaMungu tu" (5:28) [wale ambao ni mutaqqi yaani wenye Taqwa]. Hii ndio sababu imesemwa msisali nyuma ya wale ambao sala zao hata hazitafikia hadhi yakukubaliwa.'

Watu wawili walifanya Baiati. Mmoja akauliza 'inaruhusiwa kusali nyuma ya Waislamu wasio Wahmadiyya au hapana?' Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema: Wanatuita sisi makafiri. Kama sisi sio makafiri basi tuhuma za ukafiri zinawarudia wao. Mtu anayemuita Muislam kaafir anakuwa kafiri yeye mwenyewe. Hivyo imekatazwa kusali sala nyuma ya watu wa aina hiyo.

Kisha kuhusiana na aina ya watu ambao wako kimya- baadhi wanasema kuwa kuna watu ambao hawasemi chochote [dhidi ya Masihi Aliyeahidiwa (as)]. Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema:

'Wale walio kimya bali wanahesabika miongoni mwao nao hairuhusiwi kusali nyuma yao kwa sababu wanabeba ndani ya mioyo yao upinzani dhidi yetu, na ndio sababu hawajiungi nasi (ingawa hawasemi, wametukataa mioyoni mwao na ndio sababu hairuhusiwi kusali nyuma yao).

Akuzungumzia kuhusu Jamaat yake kutosali nyuma ya Waislam wasio Waahmadiyya, Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema:

'Kuweni na subira na msisali nyuma ya wasiokuwa Waahmadiyya. Hili ni jema zaidi na njia ya ucha Mungu zaidi ndani yake umo msaada wenu wa [Kimbingu] na ushindi mwishoni. Ndani ya hilo pia yamo maendeleo ya Jumuiya. Angalieni, hata katika dunia wale wasioridhika na wana hasira dhidi ya wengine hawazungumzi na wapinzani wao. Kutoridhika kwenu ni kwa ajili ya Allah Mwenyezi. Kama mtaendelea kupatana nao na kushirikiana nao, Allah Mwenyezi Hataendelea kuwaangalieni kwa Upendeleo Wake Maalum ambao Anaufanya hivyo kwa sasa. Pale jumuiya ya kiuchaMungu inapojitenga ndipo hapo inapopata maendeleo.

Tunamuomba Allah Mwenyezi Atuwezeshe kuwa wanachama waaminifu wa jumuiya hii kama inavyotakiwa na Masihi Aliyeahidiwa (as).

Mwishoni ninapenda kutoa wito wa maombi kwa Waahmadiyya wa Algeria. Hii ni Jumuiya mpya na wengi ni wanajumuiya wapya. Hata hivyo, wana imani thabiti. Siku hizi Serikali inakuwa kali sana na onevu na wanabambika kesi bila sababu na wanapeleka jela [Waahmadiyya hao]. Astaghfirullah, wanatuhumu kwamba [Waahmadiyya kule] ni sawa na Daesh. Wakati ki ukweli kama popote na katika nchi yoyote, unataka kuwapata watu wale ambao ni wenye amani na wenye kufuata sheria, hao ni wanajumuiya wa jumuiya ya Waislamu ya Ahmadiyya. Hata hivyo' nia yao ni kutulaumu tu na hivyo wanajaribu kutufananisha nao [Daesh].

Mara nyingi polisi kwa nguvu wameingia majumbani na wamejaribu kuwavua wanawake wetu hijabu zao. Kwa mfano, hivi karibuni walimuambia mwanamke mmoja kuvua hijabu yake. Alijibu, 'mnaweza kuniua, lakini kamwe sitaivua na wala sitaacha Ahmadiyyat.' Majaji kule wanatenda bila haki na wanavuka mipaka yote. Jaji mmoja alimwambia Muahmadiyya mmoja kwamba kama utaacha imani katika Ahmadiyyat, nitakuachia mara moja.' Alijibu 'Nitakufa lakini kamwe sitaacha Ahmadiyyat wala imani yangu, kwa sababu hii ni Islam ya kweli ambayo nimeigundua.' Jaji alijibu kwamba 'vizuri sana, kwa kuwa umesema hivyo nitakuhukumu kwenda jela ya maisha na utafia jela.' Alijibu 'vizuri, fanya unavyopenda'. Hivyo hii ndio hali ilivyo kule siku hizi.

Tunamuomba Allah Mwenyezi Alete wepesi kwa Waahmadiyya kule. Tunamuomba Awape uimara. Tunamuomba Awarudishie uovu wadhalimu ambao ni maadui wa Islam na Ahmadiyyat. Na tunamuomba Awajaalie *awaa* (makimbilio) Waahmadiyya wote mbali na ukatili wao. Amiin.

Bustani ya Washairi

JAMAAT KANDA YA ZIWA

1. Bismillah awali, ya pili Arrahmani,
Shinyanga mambo ni shwari, twamshukuru Manani,
Wazidi fika ukweli, hata kule ndani ndani,
Jamaat Ahmadiyya, Kanda ya ziwa ni shwari.

2. Wengi hawaiamini, Shinyanga inavyoenda,
Tena wengi wanadhani, sisi tuna unda unda,
Na hata kutoka ndani, wanazidi kutuponda,
Jamaat Ahmadiyya, Kanda ya ziwa ni shwari.

3. Hata ndani ya Jamia, tunapata upinzani,
Hawaishi kudhania, kilicho kwetu kandani,
Hususa kanda ya ziwa, namna tunavyowini,
Jamaat Ahmadiyya, Kanda ya ziwa ni shwari.

4. Nataka kuwaambia, ndungu zangu waumini,
Nuru ya Ahmadiyya, imeangaza kandani,
Katika kanda ya ziwa, Allah Ametuauni,
Jamaat Ahmadiyya, Kanda ya ziwa ni shwari.

5. Kwa fadhila za Mwenyezi, Kaing'arisha Shinyanga,
Ambaye Allah Azizi, alitakalo hupanga,
Tusaidiwe malezi, siyo kutuzongazonga,
Jamaat Ahmadiyya, Kanda ya ziwa ni shwari.

6. Na kwa ndugu zangu Suni, safari mtaipenda
Hata mgawe bikini, hamtaweza kushinda,
Hili gari la Manani, shetani hawezi panda,
Jamaat Ahmadiyya, Kanda ya ziwa ni shwari.

7. Watawala walifeli, kuizima Jumuiya,
Sembuse ninyi wawili, mwaweza kutuzuia?
Hii safari ya mbali, kenge mtaacha njia,
Jamaat Ahmadiyya, Kanda ya ziwa ni shwari.

8. Tumeshafunga mkanda, na tumeanza kupaa,
Nyie chini mnaranda, siye juu twaelea,
Ni suna yetu kushinda, sare hatujazoea,
Jamaat Ahmadiyya, Kanda ya ziwa ni shwari.

9. Yaa Rabi Mola Qudusi, tupe nguvu kemu kem,
Tuwapate wafuasi, kutoka kila sehemu,
Na utupe urahisi, mambo yawe bam bam,
Jamaat Ahmadiyya, Kanda ya ziwa ni shwari.

10. Beti kumi ni tamati, kalamu naweka chini,
Allah ikuze jamaat, izagae duniani,
Tena wajaze baiati, kama vumbi Ardhini
Jamaat kanda ya ziwa, yazidi kusonga mbele.

MWL. HAMID S. LIUCHA
SHINYANGA – SHABULUBA
(JIWE WALILOKATAA WAASHI)

WALAZE PEMA PEPONI.

1. Bismillah Karima, Mola wangu wa huruma,
Mwenye mwingi wa hekima, sifa na kila neema,
Kiumbe wako dhalima, naomba zako karama,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

2. Idd bin Ramadhani, getini alitulia,
Ukimkuta kazini, mwembeni ajisomea,
Ucheshi wake nadhani, hakuna wa kufikia,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

3. Rashid wa Msabaha, twariqa askaria,
Huyu babu alihaha, kumtafuta Masia,
Alifika na Rabuha, kuyaacha ya dunia,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

4. Al hajj Kungulilo, mnubi wa asilia,
Ukileta shalobalo, mate atakutemea,
Mtamu kupita solo, kwa kupenda jumuia,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

5. Athumani wa Makupa, Rais Dar us salaam,
Mambo mengi alitupa, pale masjid salaam,
Mzee hatokupita, hadi akupe salaam,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

6. Mbwana bin Mgunda, huyu katibu wa Mali,
Alikuwa na kiwanda, ni meneja mwenye hali,
Jamaat aliipenda, michango kila mahali,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

7. Mohamed bin Ussi, kabila ni Mswahili,
Ni mrefu na mweusi, bashasha lenye akili,
Ahubiri kwa nafasi, kwa hoja zenye mithali,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

8. Athumani Mlandula, Mluingo wa kipugura,
Hoja zake hutalala, fasaha na masikhara
Wale masheikh uchwala, wakiona wanahara,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

9. Jafa Maliki Mahamba, yeye mtoboa siri,
Mahubiri alitamba, kwa njia ya ushairi,
Hakika alijigamba, pasipo kupenda shari,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

10. Mzee Kitabu Pazi, sifa yake ya upole,
Mahubiri kama kazi, alifanya pole pole,
Aliyaweka makazi, masuni wamzodole,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

11. Ramadhani wa Marunda, Mtwara ni maskani,
Mzee alijipinda, Jumuiya iwe ndani,
Kwa kila alichotenda, Jamaat i mkononi,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

12. Mustafa Kapulilo, asiyemjua nani,
Hakutokea kilolo, Tabora unyamwezini,
Mkavu kama taulo, Jumuiya kifuani,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

13. Ally bin Ndendekile, Mikwang'ombe katokea
Kafanya hili na lile, Jumuiya kuijua,
Kawa kama msukule, kufia Ahmadia,
Walaze Pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

14. Matimbwa Hassan Ngobo, Ikwiriri wamjua
Kula yake unga robo, michango hakuchelea
Alimuhubiri sobo, kakimbilia kuvua,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

15. Mbwambwa wa Kainuza, kutoka pale Ujiji,
Alifanya miujiza, kushinda "homa ya jiji",
Masuni kuwaduwaza, hakuukubali uji,
Walaze Pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

16. Babu Rashidi Ungando, Kibiti alitulia,
Huwezi muweka kando, michango kufuatilia,
Anamjua makando, Ikwiriri kumwendea,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

17. Bakari bin Umande, Jemedari wa Kusini,
Anatembea upande, hasimami kivulini,
Mfupi kama upinde, Muulize Hamsini,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

18. Mzee Seif kumbota, pale Nyamwage mjini,
Mlemavu anasota, akiingia chooni,
Humkosi kamwe hata, Jalsa zote yu ndani,
Walaze Pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

19. Swaleh wa Kapilima, njinjo kwao katokea,
Alifanya kila hima, kuhubiri ahmadia,
Alikuwa mkulima, twawabu kujizolea,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

20. Hawa Wazee wachache, niliowatajieni,
Wengi walitema cheche, hawatoshi ukumbini,
Tuwasamehe vicheche, waje waingie ndani,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

21. Sisi kizazi cha sasa, Jukumu kubwa tunalo,
Tujipige na misasa, hili bado kubwa bwalo,
Waingie wa Mombasa, Tunduma hadi dabalo,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

22. Tamati ninamaliza, kwako Mola nakuomba,
Kila linalonitatiza, niondolee muumba,
Nijiepushe na kiza, univishe na kiremba,
Walaze pema peponi, Wazee wa Ahmadiyya.

Pazi Mazongera. (Kiumbe Mzito)
Dodoma - Jamaat

KAZI YA KUJITOLEA

1. Yamaaliki nnasi, kipenzi cha waumini,
Ikuze yangu nafasi, kujitoa maishani,
Nijaze na ikhlasi, unipandishe thamani,
Kazi ya kujitolea inahitaji subira.

2. Katika kazi ya waqfu, yahitaji ihsani,
Ihsani ya raufu, mola wa ulimwenguni,
Akupe utakatifu, na utulivu moyoni,
Kazi ya kujitolea inahitaji subira.

3. Uupate utulivu, moyoni uwe na ghera,
Na uwe mvumilivu, mwenye kuvuta subira,
Uishi kinyenyekevu, na kutenda sana birra,
Kazi ya kujitolea inahitaji subira.

4. Umlilie mwenyezi, aliyekupa nafasi,
Ili akupe malezi, kuilea yako nafsi,
Na kisha ufanye kazi, ya kuwakumbusha insi,
Kazi ya kujitolea inahitaji subira.

5. Haifai kujikweza, na kujifutua futu,
Wengine ukawabeza, ukawaona si kitu,
Pekee watoshereza, wengine vidudu mtu,
Kazi ya kujitolea inahitaji subira.

6. Pia itakuwa bora, kwa pamoja mkutane,
Na mfanye mshawara, wote mkubaliane,
Ni sunna kufanya shura, toka enzi za mtume,
Kazi ya kujitolea inahitaji subira.

7. Jambo hilo la pendeza, na litakupa thamani,
Wale unaoongoza, sana watakuthamini,
Moja ukiwaagiza, watafanya mara kumi,
Kazi ya kujitolea inahitaji subira.

8. Naikumbuka kauli, ya mtukufu masiha,
Aliyetupa habari, juu ya kujitolea,
Tusije kuibadili, Dini juu ya dunia,
Kazi ya kujitolea inahitaji subira.

9. Na wapo wanaodhani, ni kazi ya mafukara,
Bila ya ughaibuni, huwezi kuwa na hela,
Mawazo haya acheni, mtangulize akhera,
Kazi ya kujitolea inahitaji subira.

10. Tayari beti a'ashara, zimekwisha kamilika,
Allah tupe uimara, tusije tukaanguka,
Tusiwaze mshahara, ila yaumil hakka.
Kazi ya kujitolea inahitaji subira.

MWL. HAMIDU S. LIUCHA
SHINYANGA - SHABULUBA

Vita Dhidi ya Dawa za Kulevya

Kutoka uk. 2

Hadhrat Abdullah ibn Umar anasimulia kwamba Mtume s.a.w. alisema. Yeyote anayekunywa pombe Allah hatokubali sala zake / maombi yake kwa muda wa siku 40.....
(*Tirmidhi, Nasai, Ibn Majah and Daarami from Ibn Amr*)

Hadhrat Jabir anasimulia kwamba Mtume s.a.w. alisema "Chochote kinacholevya (kilicho haramu) katika uwingi wake pia ni haramu katika uchache wake. (*Tirmidhi, Abu Dawood and Ibn Majah*)

Hadhrat Ibn Umar r.a. anasimulia kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. alisema kuna watu wa aina tatu ambao hawatoingia peponi. Mlevi mzoefu, anayewaasi wazazi wake na mume asiye na hadhari anayeingiza uchafu ndani ya familia yake. (Ahmad and Nasai)
Hadhrat Ibn Abbas anasimulia kwamba Mtume s.a.w. alisema: Mlevi mzoefu anapofariki anakutana na Mola wake akiwa kama mwabudu masanamu. (Ibn Majah)

Kwa ufupi hadithi hizi na zinginezo nyingi zinaonesha upana wa ubaya wa ulevi na jinsi Mtukufu Mtume s.a.w. alivyoukataza kwa namna ambayo hakukuachwa uchochoro wowote unaoweza kumruhusu mtu kutumia ulevi wa aina moja au nyingine.
Muislamu haruhusiwi kutumia ulevi katika hali yoyote iwayo hata kama itasemwa kuwa dawa, hatoruhusiwa kutumia ulevi moja kwa moja ingawaje uwe kidogo kiasi gani.

Hivi ndivyo Uislamu ulivyofundisha na msimamo huu ndio pekee unaoweza kuondolea mbali tabia ya ulevi katika jamii.
Lakini mtindo wa watu wenye mitazamo ya kidunia tu, isiyokuwa na mwongozo sahihi kutoka kwa Mungu wa 'kuharamisha baadhi ya vileo' na 'kuhalalisha baadhi yake', mtindo huo hauwezi kamwe kuwazuia watu wasitumie vileo. Bali kwa hakika unawashajiisha zaidi kuuendea uovu huo.
Wakati ukishafungua mlango mmoja wa matumizi ya ulevi na mlevi atakapoona aina ya ulevi aliyoizoea hamfikishi tena kwenye ile hali aitafutayo basi bila shaka atafikiria kupata ulevi 'ulio bora zaidi' ili alewe vizuri zaidi.

Hivyo, tukiwa viongozi wa Dini tunaungana na serikali yetu na kila mtu anayepiga vita ulevi lakini tunalazimika kwa heshima tuwakumbushe kwamba kama kweli tunataka kupiga vita ulevi basi tupige vita ulevi wa aina zote. Uwe ulevi wa kiswahili au wa kizungu, wa kienyeji au wa kigeni wote unayo madhara na haufai kutumiwa na wanadamu. Uwe ulevi wa 'kiroba' au wa 'chupa' wote ni najisi na ni sumu isiyotakiwa kugusana na damu ya mwanadamu. Uwe ulevi wa 'unga', 'majani' au 'kinywaji' haufai kumruhusu mwanadamu kuutumia.
Lakini kama tutaendelea na fikra kwamba ulevi huu na huu ni haramu lakini huu na huu ni halali basi hapo hali yetu itakuwa ni sawa na mlevi atiaye maji ndani ya pakacha akiidhani kuwa ndoo. Hatutoweza kamwe kupambana na kushinda vita hii ya dawa za kulevya.

Nilivyojiunga na Ahmadiyya Muslim Jamaat

Kujiunga kwangu na Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya kumetokana na ushawishi wa marehemu Mzee Abubakar Hasan Abubakar ambae alikuwa mwanajumuiya wa siku nyingi na maarufu hapa Mjini Morogoro. Marehemu mzee Abubakar pia ndie alienishawishi kujiunga na Jeshi la Polisi 1954 - 1976 nilipo staafu. Halikuwa jambo rahisi kwangu kumkubalia mzee Abubakar aliponitaka nijiunge na Jamat Ahmadiyya kama nilivyomkubalia aliponishawishi kujiunga Jeshi la Polisi.

Hii ilitokana na tuhuma za wapinzani dhidi ya Ahmadiyya, kwamba makadiani ni makafiri, makadiani wanae mtume wao, na waumini wao wote wanapigwa mihuri mataKoni. Kwa upande wa pili baba yangu mzazi alikuwa mpinzani mkubwa wa Ahmadiyya na s'ababu alizokuwa akizitoa ni zile zile za 'Masuni'. Njia ya kunishawishi kujiunga na Ahmadiyya aliyotumia marehemu mzee Abubakar ilikuwa kwa kunipa vitabu vya Jumuiya kusoma, kimoja baada ya kingine. Kitabu cha Mwito Kwa Mfalme Muislam baada ya kukisoma kilimaliza kiu yangu yote katika kufikia uamuzi kama Makadiani walikuwa Waislamu au makafiri.

Niliamua kumpa baba yangu kitabu cha Mwito Kwa Mfalme Muislamu ili nae asome na kutoa maoni yake kama Makadiani kweli walikuwa makafiri au Waislamu. Baada ya mwezi mmoja nilimuuliza baba yangu juu ya kitabu nilichompa kusoma nae alinihakikishia kuwa Makadiani sio makafiri ni Waislamu. Lakini dosari yao ni juu ya huyu mtume wao,



Mzee Jumanne Rajab wa Morogoro

kwa sababu Waislamu wote duniani kote wanaamini kuwa: mtukufu Mtume s.a.w. ni mtume wa mwisho na hakuna mtume mwingine yeyote baada yake.

Ili kujiridhisha na suala: la Uislamu wa Makadiani niliamua kuitisha mjadala nyumbani kwangu kati ya sisi Masuni na Ahmadiyya, mada ikiwa kuendelea kwa Utume. Masharti yaliyo kubaliwa ni kwamba katika mjadala wote itumike Qur'an tukufu bila ya hadithi. Kwa upande wa Masuni vijana wengi walijitokeza kuzungumzia mada, na kwa upande wa Jumuiya Ahmadiyya alihudhuria Sheikh Abdurahman Khan - Sheikh wa Mkoa, na wanajumuiya wengi.

Masuni walinipendekeza mimi niwe Mwenyekiti wa dhifa ambapo kwa upande wangu ilikuwa ndio mara ya kwanza. Mzungumzaji mkuu kwa upande wa Ahmadiyya alikuwa ndugu Abdurahman Rashidi Mikila ambae aliwatoa kamasi Masuni. Aya zilizotolewa na upande wa Masuni kuwa ndio zinazofunga Utume usiendelee au mwisho wa Utume ni Sura 33:41 na Sura 5:4. Ndugu Mikila alizichambua aya zote hizo kwa kuzitolea tafsiri sahihi kinyume na tafsiri zao, kuwa aya hizo zinafunga utume usiendelee.

Katika hali ya kushindwa ya kutetea hoja Masuni waliamua kuleta ubao utumike kuandika yanayo zungumzwa lakini badala yake jambo lililojitokeza ubao huo ukawa unatumika kufundishia lugha ya kiarabu, nahau, lafidh, na mengine mengi katika lugha ya Kiarabu. Baada ya Masuni kuona jahazi linazama wakaamua bila ya haya kuanza kutoa hadithi kwa kusoma kitabu cha Mashia kiitwacho "Mtume Muhammad ni Nabii wa Mwisho".

Mimi nikiwa Mwenyekiti nilipinga kwa sababu ya kwenda kinyume na makubaliano na nikatoa maelezo kwamba kama itakubalika hadithi zitumike basi upande wa pili wa Ahamadiyya nao waruhusiwe kujibu kitabu hicho kwa kutumia kitabu chao "Muhuri wa Manabii", kitabu ambacho nilikwisha kipitia.

Kwa uamuzi wangu huo Masuni walianza kulalamika na kunishutumu kwa kusema kuwa wao walijua tokea mwanzo kuwa mimi nilikuwa mmoja miongoni mwa Makadiani kwa sababu ati nimeonesha upendeleo juu ya Ahmadiyya.

Kwa kuwadhihirishia Masuni kuwa utume katika dini ya Islamu unaendelea mpaka siku ya kiyama ndugu Mikila alitoa aya zifuatazo kwa uchache:- 37:72, 73; 22: 76; 40:35, 41:44, 72:8, 3:180, 3:82, 7:36, 37; 57:20 na 33:8. Ndugu Mikila alisisitiza kwa kusema kuwa utume uliofungwa ni ule utume wa kuleta kitabu kingine cha sheria dhidi ya Qur'an tukufu kilichoteremshwa kwa mtukufu Mtume Muhammad s.a.w na pia hao Manabii wote watakaokuja baada ya Mtume Muhammad s.a.w watatokana na umati wa Waislamu wenyewe na wala hawataongeza au kupunguza chochote kutoka mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w na Qur'an tukufu.

Baada ya mjadala kumalizika Masuni wakawa wananitembelea nyumbani kwangu na kunishawishi nirudi katika Usuni na sababu walizokuwa wakitoa ni kwamba mimi nimesoma vitabu vya upande mmoja tu - vitabu vya Ahmadiyya, hivyo walinitaka nisome na vitabu vya upande wa pili kwa maana vitabu vya Masuni.

Mimi niliwajibu kuwa kitabu ninachokijua mimi ni kimoja tu, nacho ni Qur'an tukufu ambacho ndicho ninachosoma Ahmadiyya. Masuni walikata mguu kunitembelea na kunishawishi kurudi katika Usuni baada ya mimi mwenyewe kuchangamka kutokana na elimu ya Masihi Aliyeahidiwa niliyoipata kutoka Jumuiya yake.

Nimejiunga na Jumuiya Ahmadiyya Novemba, 1997 kabla ya kifo cha marehemu baba yangu 1998. Kwa Muhtasari haya ndio maelezo yangu nilivyojiunga na Jumuiya Ahmadiyya baada ya ukweli kunidhihirikia.

Mbashiri wa kwanza Mzalendo wa kujitolea Afariki

Na Al-Ustadh Khamisi Sultan S. Wamwera – Dar es Salaam

Kwa huzuni na masikitiko makubwa sana, hivi sasa tumeondokewa na mpendwa wetu Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima Lihomba ambaye aliaga dunia mnamo tarehe 14/11/2016 usiku na kuzikwa siku ya pili saa kumi jioni kule Duthumi Morogoro. Hakika sisi sote ni wa Allah na kwake ndiko marejeo yetu.

Tuliyeishi naye tunaona anayo historia, wasifu na mengi ya kujifunza kutoka kwake. Ninamuomba Mwenyezi Mungu maandiko yangu haya yasiwe na chumvi wala yasinyunyiziwe sukari. Bali yasiwe ya ukatili nikapokonya sifa zake za kutoziandika. Ewe Mola nisaidie.

Sheikh Swaleh Mbaruku alizaliwa miaka mia m oja hivi iliyopita. Ni karne. Alizaliwa kitongoji cha Njinjo wilaya ya Kilwa mkoa wa Lindi, inasemekana mnamo mwaka 1916. Naamini Mpogoro kwa kabila. Alisoma masomo ya dini ya Kiislamu kwa waalimu na masheikh mbalimbali. Alikuwa mwana Mantiki, Fiqih, Maani na Swarfa. Watu walimwamini sana.

Katika hali ya kutafuta riziki ya halali, Sheikh Swaleh alisafiri hadi Dar es salaam mnamo mwaka 1950. Yeye alikuwa fundi mshoni wa nguo za mavazi mbalimbali. Kwa shughuli hii, pale alipokuwa anafanyia kazi palikuwa hapakosekani watu kwa mazungumzo ya dini na ya maisha ya dunia. Kwa upande mwingine, katika miaka ya 1945 hadi 1956 Jumuiyya ya Ahmadiyya hapa Dar es salaam ilikuwa na wabashiri watatu maarufu, kila mmoja kwa muhula wake. Alikuwapo Sheikh Fadhlullah Bashir, Sheikh Jalaluddin Qamar na Sheikh Abdulkarim Sharma. Sheikh Swaleh Mbaruku alipata habari za Jumuiya ya Ahmadiyya kupitia kwa Masheikh hawa watatu. Siku za mwanzoni alipozipata zikamshtua sana hususan alipoambiwa utume ni miongoni mwa neema adhimu ya Allah ambayo haina mwisho wa kuwafikia wanadamu hadi dunia itakapofikia mwisho. Neema ya utume ni kama vile ya chakula, neema ya riziki Allah Anaendelea kuwaruzuku wanadamu chakula mpaka Atakapoleta kiyama. Ndivyo vivyo hivyo Allah Ataendelea kutuma Manabii wake duniani hadi hapo Atapoifuta dunia yenyewe. Unabii ni uhai wa dini ya Kiislam. Sheikh Swaleh Mbaruku alioneshwa aya kadhaa za Qur'an Tukufu kuhusu jambo hili. Bali zaidi alielezwa kifo cha Seyidna Isa mwana wa Mariam (as) aliambiwa Nabii Isa (as) amefariki kama Manabii



Al-Ustadh Khamisi Sultan S. Wamwera

Al Marhuum Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima

wengine wala hakupaa kwenda mbinguni. Kwa hili, pia alioneshwa aya kadhaa zinazoeleza kifo cha Nabii Isa (as) na kisha akaongezewa habari kwa kuambiwa kuwa zile habari za kurejea tena Nabii Isa hapa duniani wakati wa akheri zamani zilikuwa zinamuhusu mtu mwingine na mtu huyo ni Seyidna Ahmad (as) aliyetajwa kwenye Qur'an Tukufu sura 61:7. Pamoja na maelezo haya yote, Sheikh Swaleh alipewa baadhi ya vitabu vya Jumuiyya avisome. Hakupata usingizi sawasawa. Sheikh Swaleh Mbaruku baada ya kupata maelezo hayo kutoka kwa Masheikh wa Kiahmadiyya, mwenyewe alisema yalipasuwa kichwa chake sana. Alikuwa anatanabahi khabari hizo. Hakulala usingizi wa lepe, usiku kwa saa nyingi, alikuwa anasoma vitabu alivyopewa. Kwa kuwa Sheikh Swaleh alikuwa mmoja wa wanafunzi wa sheikh Idris basi akamuendea Mwalimu wake huyo na kumweleza aliyoyapata huko mitaani. Alimweleza kuwa amezungumza na Masheikh wa Kiahmadiyya kuhusu kuendelea kwa utume na kifo cha Nabii Isa (as). Je yeye alikuwa anasema nini kwayo? Sheikh Idris hakuwa na majibu ya suala hili wala maelezo ya kumtosheleza mwanafunzi wake ila alimuonya kwa kumwambia akae nao mbali watu hao na kama kuna vitabu wamempa kuvisoma, basi avichome moto. Hao ni Makadiyani, makafiri wanaopiga mihuri matakoni. Akampa angalizo kamwe asiambatane na Ahmadiyya watampoteza. Sheikh Swaleh Mbaruku kwa mtazamo wake aliona hakupewa maelezo mutawaliya ya kuzima kiu yake ya kupata maelezo makini na swahihi kuhusu lile aliloliwakilisha kwa Mwalimu wake. Huyo mbio hadi kwa Sheikh Hassani bin Amir ambaye kwa wakati huo alikuwa anatisha. Sheikh Swaleh akamweleza Sheikh Hassan bin Amir jinsi alivyokutana na Masheikh wa Jumuiyya ya Ahmadiyya na mambo waliyozungumza. Sheikh Hassan bin Amir akatowa kauli kama ile ya Sheikh Idrisa. Tahadhari walizozitowa Sheikh Idrisa na Sheikh Hassan bin Amir hazikufuwa dafu, bali Sheikh Swaleh Mbaruku sasa akawa karibu zaidi na Masheikh wa Kiahmadiyya. Alikaa nao kwa miaka miwili hivi akijifunza mambo mbalimbali na kwa kujisomea vitabu vya Jumuiya. Baadaye, mwaka 1953, Sheikh Swaleh Mbaruku alijiunga katika Ahmadiyya kwa fadhila za Allah. Kujiunga tu Ahmadiyya, Sheikh Swaleh akajitolea kuwa Mbashiri wa Jumuiyya wa kujitegemea. Akawa jembe kweli kweli, akatumiwa vilivyo katika Tabligh. Wakati huo swala zote za faradhi zilikuwa zinaswaliwa nyumbani kwa Bwana Abdulkarim Butt, mtaa wa Kichwele ambao hivi sasa unaitwa Barabara ya Uhuru. Pamoja na kushiriki katika Tabligh na Masheikh wa wakati huo, Sheikh Swaleh alishiriki kutafuta mahala pa kujenga Msikiti. Pakapatikana hapa ulipo hivi leo Masjid Salaam. Kabla palikuwa mahala pa kutupia magoroso, malapulapu na makopo. Leo umesimama Msikiti wa ghorofa! Alhamdulillah.

KIMYA KIMYA

Mwaka 1955, Sheikh Swaleh ghafla alifunga safari ya kurejea kwao Kilwa kule Lindi. Kwa wakati ule kutoka Dar es Salaam hadi Lindi ilichukua siku tatu au nne hivi. Barabara ilikuwa ya udongo wa mfinyanzi na sehemu nyingine ni ya michanga. Miundo mbinu ya barabara haikuwa mizuri. Magari ya kusafiria yalikuwa machache mno. Sheikh akafunga safari kuelekea Kilwa. Ni asubuhi ya mwezi mtukufu wa Ramadhani anakwea basi kuelekea huko. Saa kenda gari alilopanda Sheikh linafika Rusende kule Rufiji mwisho wa safari yake. Sheikh na abiria wengine wanashuka kungojea usafiri mwingine waunganishe, lakini haukupatikana. Sheikh Swaleh akauliza mahali ulipo Msikiti. Akaonyeshwa. Akafika hapo kwa ajili ya swala na akazungumza na Imamu wa hapo. Aliyezungumza naye alikuwa Sheikh Mkuu wa Tarafa hiyo ya Rusende. Ni Sheikh Masood bin Khatibu. Sheikh Swaleh akamweleza Sheikh mwenziye huyo madhumuni ya kuwapo hapo. Alimwambia kwamba anaelekea Kilwa, lakini kwa ajili ya matatizo ya usafiri, amelazimika kukwama pale. Jinsi walivyokuwa wanaendelea kuzungumza, Sheikh Masood bin Khatib akagunduwa kwamba aliyekuwa anazungumza nae si mpumbu, bali ni mtu anayeelewa vyema mafundisho ya Islam. Akamwita mwanafunzi wake mmoja amchukue Sheikh Swaleh ampeleke kijiji cha Nyipara. Ni mipango ya Allah hakuna ajuwaye ndani kuna nini.

KIJIJI CHA NYIPARA.

Sheikh Swaleh Mbaruku anafikishwa kijiji cha Nyipara na kukutana na ndugu wachache waliokuwa Msikitini. Akajieleza kama alivyojieleza kwa Sheikh Masood bin Khatibu. Wale ndugu waliopo pale wakamwambia karibu hapa ndipo petu. Kwa kuwa jamaa wengi walikuwa makondeni, Sheikh Swaleh alisubirishwa msikitini hapo hadi jioni wengi wa wanakijiji waliporejea kutoka mashambani. Baada ya swalatul Magharib, Imam wa Msikiti wa Nyipara alisimama na kutangaza kwamba pale kwa siku ile wanaye mgeni ambaye wenyeji wangependa kujuwa habari zake kwa Baraka za mwezi mtukufu wa Ramadhani. Sheikh Swaleh Mbaruku aliwaeleza waumini hao wa Nyipara kwamba yeye yu msafiri ametoka Dar es Salaam anaelekea kwao Njinjo Kilwa kuwaona watoto wake ambao amewaacha kwa muda mrefu. Waumini wa Nyipara walipomuona Sheikh Swaleh ni msomi na muelewa wa mambo ya dini ya Kiislamu kuliko wao walivyokuwa, basi walimuomba abaki Nyipara kwa siku chache ili awape alicho nacho kuhusu dini yetu ya Kiislamu. Walimuomba ombi lao ikiwezekana likubaliwe. Sheikh Swaleh Mbaruku alikubali ombi hilo. Kwa niaba ya waumini wa kijiji, Mzee Mchawi ndugu Matimbwa alimchukuwa Sheikh na kwenda kuishi nyumbani kwake.

Kijiji cha Nyipara kilikuwa na nyumba zisizozidi mia moja. Kilikuwa kwenye barabara kuu itokayo Dar es Salaam kuelekea Kusini. Nyumba zilikuwa pande zote mbili, hapana shaka ni mtaa kamili uliojazwa na nyumba kushoto na kulia barabara ilipita katikati. Nyipara ni kijiji kilichokuwa na neema mbalimbali. Kilikuwa kimekaliwa na wakulima. Mahindi na mpunga ndicho kilimo cha chakula. Pamba na ufuta yalikuwa mazao ya biashara. Kila palipokuwa na nyumba, nyuma kulikuwa na bustani ya migomba, miembe na mipapai. Kijiji hiki kilikuwa na mabwawa makubwa ya asili mawili. Ndondonga na Mtembwe. Mabwawa ambayo yalikuwa yanawapatia kitoweo wakazi wa kijiji cha Nyipara. Ni fadhila kubwa ya Allah juu ya kijiji hiki.

HEKIMA NA BUSARA INATAKIWA.

Allah Mtukufu Anasema katika Qur'an Tukufu kwamba waitwe watu kwenye njia Yake kwa kutumia hekima, busara na mawaidha mema. Hii ni njia ambayo Sheikh Swaleh aliitumia wakati wote. Yeye sasa baada ya kukabidhiwa uongozi wa Msikiti wa Nyipara na mambo yote ya dini yetu ya Kiislamu, alianza kutayarisha darasa la Qur'an Tukufu. Kwa kuwa ulikuwa mwezi mtukufu wa Ramadhani aliliweka somo la swaumu mbele ya waumini. Aliwaambia kwamba Allah katika Qur'an Tukufu ametoa ruhusa usiku wa swaumu kukutana na wake zetu kwa sababu wao ni nguo kwetu nasi ni nguo kwao. (Suratul Baqara aya 188). Habari hizi zilistuwa watu, kwa sababu huko tulikotoka Masheikh walikuwa wanafundisha kwamba katika mwezi wa Ramadhani imeruhusiwa siku tatu tu mtu kukutana na mkewe. Kumi la kwanza siku moja, kumi la pili siku moja na kumi la mwisho siku moja basi.

WATU WENGI WAJA DARASANI.

Habari zikaanza kusambaa huko na huko kwamba Nyipara ajile Sheikh naye anafundisha mambo ya ajabu sana. Basi, watu kutoka vijiji vya karibu walianza kumiminika kuja kusoma. Katika darasa hilo, Sheikh Swaleh aliweza kueleza kifo cha Seyidna Isa (as), kuendelea kwa utume na ufikaji wa Seyidna Ahmad (as). Habari zikaenea sasa wilaya yote ya Rufiji kwamba ati wameingiliwa na watu wavurugao mafundisho ya Islam. Masheikh wa Rufiji wakafikishiwa habari hizi. Sheikh Aliy Meli, Sheikh Shamte Kilonda, Sheikh Aliy Mgomi na Yule Sheikh Masood bin Khatibu walikasirishwa mno na maelezo aliyoyatowa Sheikh Swaleh, lakini hayupo aliyejitokeza bayana kuzungumza naye.

Sheikh Swaleh akawa na kundi kubwa linalomkubali kwa sababu kila kitu alikuwa ananukuu kutoka kwenye Qur'an Tukufu na Hadithi za Mtume Mtukufu Muhammad (saw). Na ni wakati ambao Sheikh Swaleh alikuwa bado hajaeleza habari za Ahmadiyya. Lakini sasa wakati ukafika. Sheikh Swaleh akaandika barua Dar es Salaam kueleza habari za kuwepo kwake Rufiji na namna mambo yalivyo. Wakati huo Mbashiri aliyekuwaponi Sheikh Abdulkarim Sharma. Sheikh Sharma baada ya kupata barua hiyo mara moja akafanya haraka kufika Nyipara Rufiji kukutana na Sheikh Swaleh.

Itaendelea toleo Lijalo. Inshallah

Mambo Mema huwa na Mitihani Mikubwa

Na Abdillah Kombo,
Dar es Salaam

Mambo Mema huwa na Mitihani Mikubwa - Kauli hiyo imetolewa na Alhaji Abdullah Salim Seif Al-Habsy katika sherehe za ufunguzi wa msikiti mkubwa na wa kisasa, "Masjid Abubakar Sadiq" katika kijiji cha Zenethburg, Tarafa ya Bwembera wilaya ya Muheza mkoa wa Tanga hivi karibuni. Katika sherehe hizo ambazo zilihudhuriwa na waumini wa dini mbalimbali kuanzia na wanakijiji wenyewe wa Zenethburg pamoja na wa wanaumini wa vijiji vya jirani, ikiwemo vijiji cha Potwe, Mnyasi, mianga, Kihuwi nk. Sherehe hizo pia zilihudhuriwa na sheikh wa Wilaya ya Muheza Sheikh Abdullah Seif, Mbunge wa Muheza Balozi Adadi Rajabu na uongozi mzima wa serikali ya kijiji cha Zenethburg, wakiongozwa na M/Kiti wa kijiji hicho Mh. Juma Kilo.

Alhaji Abdallah Al Habsy aliendelea kusema kuwa, alikuwa na wazo la muda mrefu la ujenzi wa msikitini huo, baada ya kuona kuwa ule wa zamani mbali na kuwa mdogo, lakini pia umechoka sana, kiasi kwamba kuufanyia marekebisho ni sawa tu na kujenga mpya, aliendelea kusema, akiwa na wazo hilo hilo alipanga mipango mingi na kushaurianana watu kadhaa ili kutimiza azma yake hiyo. Mengi yalitokea katika mchakato huo, ikiwemo kupoteza pesa na vitu vya thamani kubwa, lakini hakukata tamaa bali aliendelea na juhudi yake na hatimae kwa msaada mkubwa wa M/Mungu amefanikiwa kutimiza ndoto yake na leo kwa furaha kabisa yuko hapa Zenethburg katika ufunguzi wa msikiti huu mpya na wa kisasa unaojumuisha madrasa ya kufundishia watoto kusoma Quran Tukufu na nyumba ya mwalimu.

Aliwaasa waumia kuwa makini hasa katika maswala yenye kuleta maendeleo-, kwani wakati mwengine neema inapopatikana huweza ikaja na shari zake, hivyo ni muhimu kuwa makini inapopatikana neema yeyote ile ili isije kuwa shari badala ya heri. Alisisitiza kuwa, msikitini ni nyumba ya Mwenyezi Mungu na kuwa kila mtu anaetaka kufanya ibada basi ana haki na kufanya ibada katika nyumba hiyo, aliomba uongozi wa kijiji uweke uongozi imara wa msikiti huo na kama kutakuwa na mambo madogo madogo basi uongozi huo uweze kuwa wa kwanza kuyatatua.

Akitoa salam katika sherehe hizo za uzinduzi wa msikiti huo, mbunge wa jimbo la uchaguzi la Muheza Balozi Adadi Rajabu, alisema kuwa ni vizuri kuwa na nyumba za ibada ili wananchi waweze kufanya ibada zao na kuacha kujishughulisha na mambo yasiyokuwa na lazima, au ya uvunjifu wa amani. Alisema swala la elimu kwa vijana wetu ni nguzo na ndio msingi mkubwa wa kuwarithisha vijana wetu, ili tuwe na yakini ya kuwaacha vijana wazuri wa kuendeleza yale mema ambayo tumewafunza tukiwa hai.

Alisifia kuchimbwa kwa kisima katika msitiki huo, akasema amepata taarifa kuwa tangu kisima hicho kilipochombwa, maji yamekuwa yakitoka muda wote na hivyo kusaidia sana wakaazi wa kijiji hicho kupata maji ya uhakika na kwa wakati.

Alisema tatizo la maji ni kubwa na sehemu nyingi za jimbo lake la uchaguzi zimekuwa na shida kubwa ya maji, lakini alisema jambo hilo linafanyiwa kazi na muda si mrefu hali hiyo ya shida ya maji itapungua kama si kwisha kabisa.

Akizungumzia wakati wa kuwakaribisha wageni waliohudhuria katika hafla hiyo, mwenyekiti wa kijiji cha Zenethburg Muheshimiwa Juma kilo, alisema kuwa wamepitia kwenye changamoto nyingi mpaka hatimae kufikia kukamilika kwa msikiti huo. Alisema kuwa, kulikuwa na watu ambao hawakupenda wala kuliunga mkono swala hilo, na kusema maneno yakutisha kuhusu ujenzi wa msikiti huo, lakini hatimae leo hii msikiti umesimama na wote ni mashahidi kuwa kazi ngumu na kubwa imefanyika mpaka kufikia hapo.

Aliowaomba waumini wote wa kijiji hicho na hata vijiji vya jirani, kuhakikisha wanautumia msikiti huo kwa lengo lililokusudiwa kufanya ibada na kumcha mwenyezi Mungu, jambo hilo likienda sambamba na utoaji wa elimu kwa watoto na watu wazima pia. Alisisitiza kuwa siku zote Umoja ni Nguvu na mkiwa wamoja mtapata maendeleo makubwa.

Sheikh na maalim wa kijiji cha Zenethburg wa muda mrefu, mzee Zuberi Hussein, katika salam zake alitoa muongozi wa kina kuhusu nidhamu na heshima ya msikiti. Huku akinukuu hadith mbalimbali za mtume mtukufu (saw) sheikh Zeber alisema, msikiti ni mahali matakatifu na kuwa nidhamu na adabu za msikiti ni kitu cha kuzingatia sana, 'si vizuri kukaa msikitini na kuanza kusema mambo mengine nje ya maswala ya ibada na kumtukuza Mwenyezi Mungu' alisisitiza sheikh Zuber.

Aliendelea kusema kuwa, kuna makosa mengi waumuni huyafanya bila kujijua na hivyo akasema kuwa kwenye hili watu hawana budi kufanya jitihada kubwa kuepukana na maswala ya aina hii, haswa wanapokuwa msikitini.

Shughuli hiyo ilipendeza kwa kusomwa kasda na wanafunzi wa madrasa hiyo ya hapo Zenethburg na kisha kufuatiwa na karam kubwa iliyofanyika vizuri mno. Baada ya karam hiyo mgeni rasmi Alhaj Abdullah Salim Seif Al Habsy alipanda miti mitano kama ishara ya uhai katika viwanja hivyo vya msikiti.



Alhaji Abdullah Salim Seif Al-Habsy akitoa hotuba katika Ufunguzi wa Msikiti katika kijiji cha Zenethburg

Kutoka Meza ya Mhariri

Mti hujulikana kwa Matunda yake

Sheikh Abdulrahman Ame sahib amedhihirisha ukweli huo wa usemi wa Nabii Isa a.s. Uwezo wake wa kufanya kazi za Jamaat kwa tabasamu bila kuchoka kulimfanya Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiya Tanzania. Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry amshauri Kiongozi mkuu wa Jamaat Ahmadiyya duniani (Khalifa Mtukufu a.t.b.a.) kwamba aliyekuwa mwalimu aweze kuwa sheikh.

Ushauri huu ulikubaliwa na Huzur na wajumbe wa Majlis Amila walipewa taarifa hiyo njema.

Gazeti la Mapenzi ya Mungu ambalo lilianzishwa miaka 80 iliyopita na ambalo Ame sahib amekuwa akilitumikia kwa muda sasa linatoa pongezi kwa mwanakamati huyo wa Bodi ya Gazeti hili na kumtakia mafanikio katika kuitumikia Jamaat.

Chema Chajiuza

Tarehe 15/2/2017 gazeti la Mapenzi ya Mungu lilipata mgeni kutoka chuo Kikuu cha Moi nchini Kenya. Mgeni huyo Bi Ana ambaye ni mwanafunzi wa Kiswahili anayesomea shahada ya uzamivu (PhD) kuhusu mshairi maarufu Mathias Mnyapala - Pendachako. Kituo chake cha kwanza bibi Ana alipofika Tanzania ilikuwa ni kwenda chuo Kikuu cha Dar es Salaam alipokutana na Prof. Mulokozi.

Katika mazungumzo yake Prof. Mulokozi alimwambia kazi yako itakuwa na upungufu mkubwa bila kufika Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Prof. Mulokozi alimpatia simu ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya na akaweza kufika hapa ambapo alikutana na Bw. Muhammad Manoro ambaye alimfahamu vilivyo Mathias Mnyampala na jitihada zinafanyika pia ili aweze kukutana na Al-Ustadh Khamis Wamwera ambaye walijibizana na Mathias Mnyampala katika ule utenzi maarufu wa Injili.

Baada ya mazungumzo hayo Mhariri wa Mapenzi ya Mungu alimpatia nakala kadhaa za gazeti hilo na alishukuru sana.

Redio Ahmadiyya Yaja

Kwa miaka kadhaa sasa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini imekuwa na kilio cha kuwa na shule ya sekondari na Redio. Shukurani zote ni za Allah kwani kwa hivi tunayo shule ya sekondari na Inshallah harakati zinaendelea za kuwa na Redio yetu itayojulikana kama Redio Ahmadiyya.

Habari hizi njema zilitolewa na Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry katika maadhimisho ya siku ya Mwana Aliyeahidiwa r.a. yaliyofanyika katika msikiti wa Makao Makuu Dar es Salaam. Amir alisema tayari tumepata usajili wa vifaa vya redio ambavyo viko njiani.

Redio hiyo ya kwanza ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania inajengwa Mkoani Mtwara na inatarajiwa kuanza kuwatumikia Wananchi wa Tanzania kuanzia mwezi Juni 2017.

Tunaombwa maombi yetu ili Redio hii iweze kufanikiwa.

Maadhimisho ya Mwana Aliyeahidiwa yafana Dar es Salaam

Kutoka uk. 12

kutoka pande zote. Siku hizo zilipokwisha yeye alitangaza ya kwamba Mwenyezi Mungu amekubali maombi yake na ameahidi kuonyesha ishara. Akitoa tangazo juu ya ishara hiyo, Masihi Aliyeahidiwa alitangaza ya kuwa Mwenyezi Mungu alimwambia:

"Ninakupa Ishara ya Rehema Yangu kwa kuyajibu maombi yako. Nimeyasikia maombi yako na nimekirimu dua zako kwa ukubali Wangu kwa njia ya rehema Yangu na nimeibariki safari yako hii. Ishara ya Qudra na uwezo, ukarimu, ukaribu Nami inatolewa kwako, Ishara ya rehema na ihsani inaletwa kwako na unapewa ufunguo wa ufaulu na ushindi. Amani iko juu yako, Ewe mshindi. Hivi ndivyo Asemavyo Mwenyezi Mungu ili kwamba wale wanaotamani uzima waokolewe katika mkamato wa mauti na wale waliolala makaburini wafufuliwe na ili kwamba utukufu wa Islamu na heshima ya neno la Mungu Mwenye enzi idhihirike mbele ya watu na ili kwamba ukweli uwasili pamoja na baraka zake zote , na uongo utoweke pamoja na nuksi zake zote, na ili kwamba watu waweze kuelewa ya kwamba Mimi ni Mwenye Nguvu, Ninafanya N ipendavyo, na ili kwamba wawe na yakini ya kuwa Mimi Niko pamoja nawe, na ili kwamba wale wasiomwamini Mungu Mwenye enzi na wanakana na kukataa Dini Yake na Kitabu Chake na Mjumbe Wake Mtakatifu Muhammad, Mteule (amani iwe juu yake) wakabiliane na Ishara iliyo wazi na ili njia ya wakosefu iweze kubainika."

"Basi furahi ya kwamba utajaaliwa mtoto mwanamume mtakatifu na mzuri, utampokea kijana mwana ambaye atakuwa ni mbegu yako na kizazi chako. Kijana mzuri na mtakatifu atakuja kama mgeni wako. Jina lake ni lmanueli na Bashir. Amejazwa roho takatifu, na ameepukana na uchafu wote. Ni nuru ya Allah. Amebarikiwa yule ajaye kutoka mbinguni. Atafuatana na rehema ambayo itawasili pamoja naye. Atahusishwa na utukufu, ukuu na utajiri. Atakuja duniani na atawaponya wengi wenye maradhi kwa njia ya sifa zake za Umasihi na kwa njia ya baraka za Roho ya kweli. Yeye ni Neno la Allah kwani ukarimu na heshima ya Allah imemtuma na Neno la Utukufu. Atakuwa na akili sana mno na ufahamu na atakuwa mpole wa moyo na atajazwa elimu ya nje na ndani. Atawafanya watatu kuwa wanne (hii maana yake haikubainishwa). Ni Jumatatu. Jumatatu iliyobarikiwa. Mwana wa kiume, furaha ya moyo, aliyenyanyuliwa, mtukufu, mdhihirishaji wa Aliye ni wa Mwanzo na Mwisho, alama ya Yule Aliye Mkweli na wa Juu; kana kwamba Allah Ameshuka kutoka mbinguni. Kufika kwake kutabarikiwa sana sana na kutakuwa sababu ya kudhihirika kwa Jalali ya Uungu. Nuru inakuja, nuru hasa, nuru iliyosingwa na Mwenyezi Mungu uturi wa mapenzi Yake. Tutampulizia roho Yetu, atahifadhiwa chini ya kivuli cha Mwenyezi Mungu. Atakua upesiupesi katika umbo na atakuwa sababu ya kukombolewa wale walio utumwani. Atajulikana mpaka pembe za dunia na mataifa yatabarikiwa kwa ajili yake. Ndipo atachukuliwa juu mbinguni kwenda mahali alipotayarishiwa na jambo hili limekwisha katwa. (Tangazo la tarehe 20 Februari, 1886).

Ili kuthibitisha ufuulu wa Mwana Aliyeahidiwa a.s. ikiwa ni utimilifu wa bishara hiyo, Sheikh Ame sahib alieleza historia ya Hadhrta Musleh Mauud r.a. kwa ufupi:

1886: Ufunuo wa Maishi Aliyeahidiwa a.s. juu ya Mwana wa ahadi
1889: Mwana azaliwa (12 Januari). miaka 3 baada ya ufunuo.
1897:Sherehe za kumaliza kusoma Qur'an Tukufu kwa matini
1898:Mwana aanza masomo katika Taalimul-ul-Islam
1899:Alichukua baiat kwa mkono wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.
1902:Ndoa yake ya kwanza
1905:Alifanya mitihani ya serikali (matriculation)
1906:Ateuliwa kuwa Mjumbe wa Sadr-Anjuman-Ahmadiyya
1906:Mhariri wa gazeti la Tashheez-ul-Azhan
1906:Atoa hotuba ya mwanzo mkutanoni.
1907: Atoa ahadi ya kihistoria mbele ya mwili wa baba yake
1911:Aanzisha Ansarullah
1913:Achapa Al-Fazal
1914:Achaguliwa kuwa Khalifa
1914 :Aanza darsa ya Qur'an tukufu
1914:Aanzisha Majlis Shura
1914:Aanzisha Jumuiya Uingereza
1915:Jumuia Ceylon na Mauritus
1916:Umalizaji wa Minaratul Masih huko Qadiani
1921:Mahubiri Amerika na Afrika
1922 Majlis Shura yaendelea kila mwaka
1923:Lajna Imaullah yaanzishwa
1923:Upanuzi wa Masjid Aqsa Qadiani
1924:Vita dhidi ya mwendeleo wa Shudhi katika India
1924:Safari ya kwanza Uingereza
1924:Jiwe la Msingi - London Mosque
1924:Kuhudhuria mkutano wa dini zote Uingereza
1925 Kuanzishwa kwa idara ya Qadhaa katika Jumuiya
1926:Kuanzishwa kwa mkutano wa kila mwaka kwa Lajna
1926:Kuchapwa kwa Misbah - gazeti la akina mama.
1928:Kuanzishwa kwa shule ya wasichana
1928:Mwanzo wa mpango wa maisha ya Mtume s.a.w.
1931: Raisi wa All-India-Kashmir Committee
1934: Mwanzo wa Tahrik Jadid
1938 Khuddamul Ahmadiyya yaanzishwa
1938:Atfalul Ahmadiyya yaanzishwa
1938:Silver Jublee ya Khalifa wa pili
1940:Kalenda ya Kihijra itumiayo mwaka wa kijua - tangu hijra ya Mtukufu Mtume s.a.w.
1944:Madai ya uwana wa ahadi
1944:Hotuba za Hadhara katika Hoshiarpur, Ludhiana na Lahore
1944:Aanzisha chuo cha Taalimul Islam
1945:Makundi ya wahubiri yatumwa Ulaya na nchi zingine
1946:Chuo cha Uchunguzi fazle-Umar chaanzishwa
1946: Qur'an yatafsiriwa katika lugha 8
1947:Kuhama kutoka Qadiani - kwenda Pakistan.
1948: Makazi Mapya -Rabwah
1949 Khalifa ahamia Rabwah
1951:Chuo cha wasichana chaanzishwa
1953:Vurugu dhidi ya Ahmadiyya
1954:Khalifa ashambuliwa kwa kisu
1954:Qur'an yafasiriwa kwa Kidachi
1955:Ugonjwa na Safari ya pili Ulaya
1956:Wanafiki waliojitenga na kushindwa kwao na kudhalilika kwao.
1957: Tafsir Saghir yachapishwa
1959 Tafasiri ya Qur'an kwa Kijerumani (edition ya pili).
1960 Kuanzishwa kwa bodi ya Nigran
1961 Tafsiri ya Qur'an kwa lugha sita zaidi
1962 Tafsir Kabir kwa Kiingereza yamalizika
1963 Jumuiya yakuwa zaidi Afrika, wabashiri zaidi watumwa
1964 Ugonjwa waendelea
1965. Tarehe 8 November mwaka 1965 alifariki dunia mnamo saa nane na dakika ishirini za usiku.

Naye Amir na Mbashiri Mkuu akifunga maadhimisho hayo aliwakumbusha wahudhuriaji kuhakikisha wanshikamana na mafundisho ya Jamaat ili kuweza kufaidika na baraka za Mwana Aliyeahidiwa a.s. Alisema kwamba kimsingi maendeleo yote ya upanukaji wa Jamaat tunayoyaona leo, ikiwemo jamaat yetu ya Tanzania yanaweza kunasibishwa moja kwa moja na Mwana Aliyeahidiwa kwani yeye ndiye aliyeanzisha mifumo iliyousaidia ujumbe huu kusambaa duniani kote.

Aidha aliwakumbusha wanajumuiya kuhakikisha kwamba tunashikamana pamoja kwani hiyo ndio njia pekee itakayotuwezesha kukamilisha majukumu yetu makubwa.

Maadhimiso hayo yalifungwa kwa maombi yaliyoongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu.

Khuddam washiriki zoezi la Uchangiaji Damu

Na Mwandishi Wetu,
Dar es Salaam



Sehemu ya Khuddamul Ahmadiyya walioshiriki katika zoezi la uchangiaji damu salama

Kwa fadhila za Allah, Majlis Khuddamul Ahmadiyya Ilaqa (Mkoa) ya Dar es salaam wamefanikisha tukio la uchangiaji damu lililofanyika katika Ofisi za Damu Salama kanda ya Mashariki kama lilivyotangazwa hapo kabla.

Tukio hilo lenye Baraka lilihudhuriwa na Khuddam wapatao ishirini na nne (24) wa mkoa wa Dar Es Salaam, akiwemo Sadr Majlis, bwana Ramadhani Nauja sambamba na baadhi ya wana Majlis Mulk ambao kwa pamoja walikusanyika katika maeneo ya Msimbazi Center yalipo makao makuu ya Damu Salama kanda ya Mashariki, Ilala jijini Dar Es Salaam.

Zoezi la utoaji damu liliambatana na kikao kifupi baina ya msafara wa Majlis khuddam pamoja na uongozi wa Damu Salama kanda ya Mashariki ambacho kililenga katika kufahamiana baina ya pande hizo mbili sambamba na kuzijadili changamoto mbalimbali zilizopo baina yao katika suala zima la Uchangiaji wa Damu katika mkoa wa Dar es Salaam.

Kabla ya zoezi la utoaji damu kuanza rasmi, washiriki wote walipata fursa ya kutembelea ofisi na idara mbalimbali zilizopo makao makuu ya Damu Salama ambapo walipata maelezo ya kina juu ya shughuli inayofanywa na kila idara/ofisi hizo ikiwemo ile ya uchakataji wa damu kwa ajili ya kuzipanga katika makundi mbalimbali kwa ajili ya matumizi pindi zinapohitajika.

Zoezi la uchangiaji damu lilianza rasmi majira ya saa mbili kamili za asubuhi na kumalizika saa tano na nusu asubuhi ambapo Sadr Majlis alipata fursa ya kuwashukuru ndugu wote walioitikia wito na kuambatana nae katika zoezi hilo na kutoa wito kwa khuddam kuendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali za kujitolea zinazoandaliwa na tanzimu pamoja na jamaat kwa ujumla.

SHURA YA KITAIFA 2017

Amir Sahib - Jamaat Ahmadiyya Tanzania, anapenda kuwakumbusha Masheikh wa Mikoa, Marais wa Mikoa, Marais wa matawi, Walimu wa Jamaat nchini na Wanajumuiya wote kwa ujumla kwamba sawa na kalenda ya matukio ya Jumuiya ya mwaka 2016/17, Majlis Shura ya Kitaifa itafanyika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga - Dar es Salaam, siku za Jumamosi na Jumapili tarehe 29 na 30 Aprili 2017.

Matawi yote yanatakiwa yafanye vikao vya kupendekeza ajenda za Shura pamoja na kuchagua wajumbe wa kuyawakilisha matawi yao kwenye Shura hiyo ya Kitaifa. Tawi lililo na wachangiaji zaidi ya 50, linaruhusiwa kuchagua mjumbe wa ziada kwa kila wachangiaji 50 wanaoongezeka.

Marais wote wa mikoa wanahimizwa kushiriki kwenye Shura hiyo kwa gharama zao wenyewe.

Pamoja na mjumbe wa Shura atakayechaguliwa kutoka kila tawi, rais wa tawi naye pia anatakiwa ashiriki kwenye Shura ya mwaka huu.

Wajumbe wote wanatakiwa wawe wamefika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga Dar es Salaam jioni ya siku ya Ijumaa tarehe 29 April 2017.

Ishara ya ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Kutoka uk. 12

Musleh-e-Maud (ra) alisema ni wangapi katika orodha hii walitoa tangazo kuwa ni wajadid? Masihi Aliyeahidiwa (as) yeye mwenyewe alisema kwamba Aurengzab [Mfalme wa Mughal] alionekana kana kwamba ni mujadid wa zama zake. Umar bin Abdul Aziz anasemwa kuwa alikuwa ni Mujadid lakini naye pia kamwe hakudai au kutangaza kuwa hivyo. Tangazo linatakiwa kwa Mujadid aliyepewa rasmi kazi hiyo, kama vile Masihi Aliyeahidiwa (as). Kwa Mujadid asiyeteuliwa, kudai sio la lazima.

Hazrat Musleh-e-Maud (ra) alielezea zaidi kwamba hii ndio sababu hakuhitaji kufanya tangazo. Alisema wanajamaat wasihamaki kutokana na matusi ya wapinzani wa jambo hili. Matusi yao, kashfa zao na kujaribu kutudhalilisha hakujalishi kitu kwani mtu anaweza kuwadhalilisha wengine, lakini heshima ya kweli inatolewa mbele ya mahakama ya Allah Mwenye Enzi. Yule anayetembea katika njia ya Allah anapewa heshima mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu, bila kujali dharau za watu. Mtu anayetoa madai ya uongo anaweza kupata mafanikio hapa duniani, lakini ni lazima hatimae aanguke kwa sababu hana heshima ya Mungu. Akasema kwamba, kwa hivyo katika mambo yote yawe ya kisekula au ya kiroho mtu daima ashikamane na ukweli. Na njia ya kuwapima watu ni kuangalia msaada wanaoupata kutoka kwa Mungu Mwenye Enzi.

Hata hivyo, pamoja na yote haya, mara tu Mwenyezi Mungu alipomuamuru kufanya tangazo - hapo hapo alitangaza kwamba yeye ndiye Mwana Aliyeahidiwa.
Huzur a.t.b.a. anasema kwamba alipofanya dai hili, hakukimbilia tu kusimama na kutangaza kwa ufahari kwamba alikuwa ni Mwana Aliyeahidiwa. Bali alisema kwamba sawa na asili yake ilikuwa ni vigumu sana kwake kufanya hivyo. Wakati alipotangaza kwamba Mungu Amemuambia bishara imetimizwa waziwazi katika dhati yake, kwa upande mmoja wanajumuiya walikuwa na furaha. Lakini kwa upande mwingine, Ghair Mubaieen (wale waliokataa kufanya Baiat ya Ukhalifa) walianza upinzani wao.

Katika Jalsa salana ya mwaka 1945, Hazrat Musleh-e-Ma'uud (ra) alizungumzia upinzani huu na bil husus msimamo wa Maulana Muhammad Ali. Hazrat Musleh Mau'uud (ra) alisema kwamba tokea Alipofanywa atangaze kuwa ndiye Mwana Aliyeahidiwa, Maulana Muhammad Ali ameanza bila sababu kumpinga. Hazrat Musleh Mau'uud (ra) alisema kwamba ametoa dai lake kwa kufuata funuo, njozi na Utashi wa Allah. Lakini Maulana Muhammad Ali hakuweza kuleta njozi yoyote au ufunuo ulio kinyume cha hayo kukanusha madai yake. Ushahidi pekee alioutoa Maulana Muhammad Ali ulikuwa ni ufunuo wa miaka 30 iliyopita, ambao ulithibitishwa kuwa sio sahihi ki muktadha.

Ili wajithibitishe kuwa ni wakweli maadui wa mitume wanadai kwamba funuo walizopewa mitume wamejitungia wenyewe. Wayahudi na Wakristo walitoa shutuma za aina hiyohiyo dhidi ya Mtume Mtukufu (saw) pia. Hazrat Musleh Mau'uud (ra) anasema kwamba ni ajabu kwa nini Mungu hakuwapa funuo za kweli Wayahudi na Wakristo kinyume na Mtume Mtukufu (saw), ili kubainisha ni kundi gani lenye kosa.

Hazrat Musleh Mau'uud (ra) anasema kwamba hata leo, Maulvi Muhammad Ali Sahib ametoa shutuma hizohizo kwamba funuo zilizofunuliwa kwangu ni za uwongo. Kwa nini Mungu Mwenyezi Hajamfunulia wahyi wowote wa kweli Maulvi Sahib ili kufumbua ni yupi miongoni mwetu anayesema ukweli?
Kisha Huzur a.t.b.a. alitoa funuo chache alizofunuliwa Hazrat Musleh Mau'uud (ra) ambazo zinathibitisha kwamba alikuwa ndiye Mwana Aliyeahidiwa (ra).

Ya kwanza ilitokea wakati wa Masihi Aliyeahidiwa (as), ambao Masihi Aliyeahidiwa (as) aliuandika kwenye shajara (dayari) yake ambayo alikuwa akiandika humo funuo alizofunuliwa yeye. Funuo hiyo ilikuwa hivi: "Hakika, Nitawafanya wafuasi wako wawe washindi juu ya wale waliokukataa mpaka siku ya kiyama" Hazrat Musleh Mau'uud (ra) anasema kwamba kuna maana za kina katika ufunuo huu kwamba ufunuo huu unafanana na ule aliofunuliwa Yesu (as) kama ulivyotajwa ndani ya Qur'an tukufu. Lakini maneno ya huu ni: "Na nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokataa, mpaka siku ya Kiyama". Hii ni kwa sababu madai ya Yesu (as) yalikuwa ni Mtume wa mwisho katika silsila ya Musa (as). Katika hali hiyo watu wanapinga madai hayo, kisha ni baada ya kipindi cha muda mrefu watu ndio wanamkubali Mtume huyo. Lakini Mungu Mwenyezi Alipenda kunyanyua madai ya Musleh Mau'uud (ra) kufikia hadhi ya Ukhalifa, na Khalifa anarithi jumuiya mara moja, na hiyo ndio sababu maneno "Na nitaweweka wale watu" hayakuwa na haja. Hivyo kwa kutaja kwenye ufunuo kwamba "Hakika, Nitawafanya wafuasi wako washindi juu ya wale waliokukataa mpaka siku ya Kiyama", Mungu Mwenyezi Alionyesha kwamba muda fulani katika akheri zaman Atampa [yaani Hazrat Musleh Mau'uud (ra)] jumuiya muasasa (iliyokwisha simama), ambayo itaimarishwa na Mungu Mwenyezi.

Maneno "Nitawafanya wale waliokuamini…" kama yalivyotajwa ndani ya Qur'an tukufu hayakuhitajika hapa kwa sababu kutakuwa hakuna haja kuwasubiri watu waukubali ujumbe. Pamoja na ukweli kwamba maadui watapanga kuiangamiza, na watajaribu ukomo wa uwezo wao kuleta dhoruba ya upinzani, lakini bado Mungu Mwenyezi, Atampa [yaani Hazrat Musleh Mau'uud (ra)] jumuiya muasasa na Atahakikisha maadui wao wanasagwa.

Mapeghami [wale waliokataa kufanya baiati katika mikono ya Hazrat Musleh Mau'uud (ra) na wakaunda jumuiya yao] wanadai kwamba Hazrat Musleh Mau'uud (ra) alitoa madai yake kwa kutegemea njozi moja aliyoiona. Hazrat Musleh Mau'uud (ra) amesema kwamba hiyo haikuwa njozi, kwani ilikuwa na maneno yaliyofunuliwa; ulikuwa ni ufunuo uliopokelewa zaidi ya miaka 40 iliyopita.

Ishara ya pili iliyofunuliwa kwa Hazrat Musleh Mau'uud (ra) ambayo inadokeza kuwa yeye ndiye Mwana Aliyeahidiwa aliipata katika Kashf. Hazrat Musleh Mau'uud (ra) anasema kwamba alipokuwa katika hali ya Kashf, aliona kwamba amepewa bahasha iliyoandikwa majina mawili, *Muhiy-ud-diin* na *Muin-ud-diin*. *Muhiy-ud-diin* linamrejea Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye amekuja kuhuisha Islam na *Muin-ud-diin* linamrejea Hazrat Musleh Mau'uud (ra) ambaye amekuja kuauni na kusaidia katika daawa ya Islam.

Ishara ya tatu ambayo Hazrat Musleh Mau'uud (ra) aliitaja ulikuwa ni ufunuo alioupata. Ufunuo ulikuwa unasema, "Ewe uzao wa Daud! Shikamana na Amri za Allah Mwenyezi ukiwa mwenye shukurani kwake" Hazrat Musleh Mau'uud (ra) anasema kwamba kwa kutamka "uzao wa Daud", Allah Mwenyezi amemfananisha na Hadhrat Suleiman (as). Hadhrat Suleiman (as) alikuwa Khalifa baada ya Hadhrat Daud (as) na pia alikuwa ni mtoto wake.
Hazrat Musleh Mau'uud (ra) anasema kwamba ishara ya nne inayothibitisha kuwa yeye ndiye Mwana Aliyeahidiwa (ra) ni Kashf aliyoipata. Katika kashf hii, aliona kwamba alikuwa akisali katika Bait-ul-Dua [chumba kidogo ambamo Masihi Aliyahidiwa (as) alikuwa akifanya maombi] ambapo ghafla iliwekwa wazi kwa Hazrat Musleh Mau'uud (ra) kwamba Masihi Aliyeahidiwa alikuwa ni Ibrahim. Ilifunuliwa kwake pia kwamba ma-Ibrahim wengi wengine wametokea katika Umma huu [wafuasi wa Mtume Mtukufu (saw)], kwa mfano alifahamishwa kwamba Hazrat Khalifatul Masih I (ra) alikuwa pia ni Ibrahim. Kisha Hazrat Musleh Mau'uud (ra) aliambiwa kwamba yeye pia ni Ibrahim.

Hazrat Musleh Mau'uud (ra) anasema kwamba ishara ya tano iliyofunuliwa kwake ilikuwa ni katika ndoto aliyoipata wakati wa karibu na kifo cha Masihi Aliyeahidiwa (as) Hazrat Musleh Mau'uud (ra) alimuona malaika katika njozi na akamwambia Hazrat Musleh Mau'uud (ra) kwamba atamfundisha sherehe ya Sura Al-Fatiha. Malaika alisema kwamba mpaka sasa washehereshaji wote wa Qur'an tukufu wameandika sherehe mpaka kufikia maneno *Yaum-e-Diin* tu, lakini atamfundisha Hazrat Musleh Mau'uud (ra) sherehe kamili ya Surah Al-Faatiha. Hazrat Musleh Mau'uud (ra) anasema kwamba alipoamka, hakukikumbuka tena kile malaika alichomfundisha. Hata hivyo, kutokea siku hiyo, Allah Mwenyezi Amemfundisha Hazrat Musleh Mau'uud (ra) maana za ndani na za kistadi za Surah Al-Faatiha zisizo na hesabu. Kwa hakika, Hazrat Musleh Mau'uud (ra) anasema kwamba Allah Mwenyezi Amemfundisha mpangilio mpana kuhusiana na Surah Al-Faatiha ili kuthibitisha utukufu wa Islam. Hivyo, maana ya kweli ya njozi hii ilikuwa kwamba utambuzi kwa ujumla wa Qur'an tukufu na bilhusus maana ya Surah Al-Faatiha umepewa kwa Hazrat Musleh Mau'uud (ra).

Hazrat Musleh Mau'uud (ra) pia anasema kwamba alipokea ufunuo, "Hakika tutawaangamiza."
Wale waliojitenga na Jamaat wakati huo walidai kuwa ndio wengi wanaofanya asilimia 95 ya Jamaat.
Hasa, hii ilithibitika kuwa ndio ilivyotokea na Khawaja Kamal-ul-Din Sahib kabla ya kufa kwake alikubali kwamba ufunuo wa Hazrat Musleh Mau'uud (ra) bila shaka ulitimizwa na wao waliangamizwa.

Hazrat Musleh Mau'uud (ra) anasema kwamba Allah Mwenyezi Amemfunulia ishara zisizo na hesabu ambazo zinathibitisha kuwa bishara hii ilitimizwa katika dhati yake.

Huzur alihitimisha kwa kusema kwamba katika siku zijazo Jalsa nyingi zitafanyika katika kusheherekea kutimizwa kwa bishara hii katika Jumuiya na pia mipango mingi itatangazwa katika MTA. Wanajumuiya wafanye jitihada kubwa kabisa kuhudhuria na kusikiliza mipango hiyo ili kujenga uelewa wa kina wa bishara hii. Kuna ishara zisizo hesabika zilizotajwa katika bishara hii na zote zimetimizwa kwa Hazrat Musleh Mau'uud (ra) kwa utukufu mkubwa.

MAKALA ZINAHITAJIKA

Bodi ya Uhariri ya Gazeti letu tulipendalo "Mapenzi ya Mungu" inawaomba ndugu wote kwamba wajitahidi kuleta makala kwa ajili ya kulipamba Gazeti letu.

Ieleweke kwamba Gazeti letu ni la kuelimisha kwa mada mbalimbali. Hivyo kwa kadri mada zinapokuwa nyingi na za kuvutia ndipo litakapokuwa na mvuto zaidi. Pia ni muhimu taarifa mbalimbali zinazotokea Mikoani ziletwe. Kwa wale wote wanaopenda picha zao zitokee kwenye gazeti watuletee nakala ya picha zao.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Jumadil Awwal 1438 AH | FEBRUARI 2017 | Tabligh 1396 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Hadhrat Ibn Abbas anasimulia kwamba Mtume s.a.w. alisema:- Mlevi mzoefu anapofariki anakutana na Mola wake akiwa kama mwabudu masanamu. (*Ibn Majah*)

Musleh Mauud r.a. ni Ishara ya ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.

**Na Mwandishi Wetu,
Dar es Salaam**

Huzur a.t.b.a. alizungumzia juu ya bishara iongezayo imani ya Musleh-e-Ma'uud [Mwana Aliyeahidiwa (ra)] na akasema kwamba kutimizwa kwake kulikuwa ni ushahidi mzito wa ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s.).

Baada ya *Tashahhud, Taa'udh* na *Surat Fatihah* Huzur (atba) alisema:

Waahmadiyya wanaijua vizuri siku ya tarehe 20 Februari kuwa inahusiana na bishara hii adhimu. Katika siku hii Masihi Aliyeahidiwa (as) alipewa habari njema katika ufunuo juu ya kuzaliwa kwa mtoto



Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad - Musleh Mauud, Khalifatul Masih II r.a.

wa kiume ambaye atakuwa na sifa kemkem. Pamoja na mambo mengine ilitabiriwa kwamba Jamaat (Jumuiya ya Ahmadiyya) itapata maendeleo ya kipekee katika zama za Mwana huyu wa Ahadi (ra).

Huzur alisema kwamba leo atatoa nukuu kutoka katika maneno ya Hazrat Musleh-e-Ma'uud (ra) mwenyewe ambayo yananuururisha (yanatoa mwanga) ni jinsi gani bishara hii imetimizwa katika dhati yake.

Katika mwaka 1914 Musleh-e-Ma'uud (ra) alithibitishwa na Mungu kwa joho la Ukhalifa. Ilikuwa ni miaka 30 baadae - mwaka 1944 - ambapo alitangaza kwamba ametimiza bishara ya Mwana Aliyeahidiwa (ra). Hata kabla, wasomi wengi wa Jamaat na wanajumuiya kwa ujumla walihisi kwamba bishara hiyo imetimizwa katika dhati yake, na walimhimiza kutangaza kwamba alikuwa ndiye Musleh-e-Ma'uud (ra).

Hazrat Musleh-e-Maud (ra) aliwajibu kwamba kama bishara ilionekana kutimia katika dhati yake, basi iacheni iwe hivyo, lakini kulikuwa na haja gani kwake kutoa tangazo? Alitaja kwamba katika tukio moja, orodha ya Wajadid wa Islam waliopita ilichapishwa na orodha hii ilichapishwa baada ya Masihi Aliyeahidiwa (as) kuwa ameisha iona. Hazrat

Endelea uk. 11

Maadhimisho ya Mwana Aliyeahidiwa yafana Dar es Salaam

Amir sahib Aagiza mshikamano zaidi

**Na Mwandishi Wetu,
Dar es Salaam**

Kwa fadhili za Allah maadhimisho ya siku ya Mwana Aliyeahidiwa 2017 yalifanyika kwa mafanikio makubwa katika mkoa wa Dar es salaam.

Kwa kuzingatia ujenzi wa Makao Makuu unaoendelea maadhimiso hayo yalipangwa kufanyika kwenye vituo saba ambavyo ni Kitonga, Kitanga, Mbagala Nzasa, Magomeni, Kitunda, Kivule na Mnazimmoja ambapo maadhimisho hayo yalichukua sura ya kimkoa.

Maadhimisho hayo yalifunguliwa kwa usomaji wa Quran tukufu iliyosomwa na Mwl. Yusuf Mwishehe na kisha likafuata shairi lililoimbwa na Bw. Nasir Ndembo.

Hotuba ya Maadhimisho hayo ambayo ilipangwa kimsingi kuwa moja tu ilitolewa na Abdulrahman Ame sahib ambaye alianza hotuba yake kwa kuwakumbusha wasilikilizaji kwamba lengo la kuadhimisha hafla kama hizi ni kukumbuka ishara zilizomo kwenye maisha ya waja watakatifu wa Allah na kwamba kwa kupitia maisha yao tunapata ibra ya uwepo wa Allah pamoja na kupata mwongozo na rehema tukiwa waaminio.



Amir na Mbashiri Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akitoa hotuba katika maadhimisho ya siku ya Mwana Aliyeahidiwa r.a yaliyofanyika Masjid Salaam. Kuliani kwake ni Abdulrahman Ame sahib akitoa tafsiri ya hotuba hiyo.

Aliwaeleza wasikilizaji kwamba lengo la kutumwa kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. lilikuwa ni kuja kuyasafisha mafundisho ya dini tukufu ya Islam baada ya kuachwa sawa na bishara za Mtukufu Mtume s.a.w.

Alisema katika kukamilisha kazi hiyo Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa watu wa dini zingine na hasa kutoka kwa Masheikh wa Kiislam waliomdhania vibaya kwamba eti amekuja kuwapotosha watu.

Katika hali hiyo Masihi Aliyeahidiwa a.s. akaona haja kuuomba sana msaada wa Mwenyezi Mungu. Ndipo mnamo mwaka 1886 (A.D.) aliondoka kwao Qadian na akaenda mji mwingine wa Panjab uitwao Hoshiar Pur ili kumwomba Mwenyezi Mungu Aonyeshe ishara ya kuisaidia Dini ya Islam. Huko aliendelea kuomba kwa muda wa siku 40 mfululizo. Katika siku hizo Seyyidna Ahmad, (Masihi Aliyeahidiwa a.s.) alilia sana mbele ya Mwenyezi Mungu kwa kuona unyonge wa Uislamu na jinsi Dini hii tukufu ilivyoshambuliwa na maadui

Endelea uk. 10